Nipashe
Jumamosi Mei 8, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580574
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

**Mbaroni** tuhuma kumuua mkewe kisa kutumia ARV

UKURASA 3



**Nyaraka** za uongo zatikisa fidia ya bima

UKURASA 5




UKURASA 11

# Cheche za Samia kikao wazee Dar

• **Atangaza** mabadiliko makubwa serikalini bila kujali vyama, aonya majambazi ‘kupima maji kwa miguu’... *Endelea ukurasa 2*



Rais Samia Suluhu akizungumza na wazee wa Mkoa wa Dar es Salaam, Ukumbi wa Mlimani City, jana. **PICHA: IKULU**

## Wapoteza maisha kwa kuunguzwa uji wa chuma

UKURASA 4



Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play · App Store

## Mashirika manane yakalia kuti kavu

UKURASA 3

**MICHEZO** **WATANI KUMALIZA UBISHI LEO** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

## ... Wazee wampa madukuduku yao

**Na Romana Mallya**

WAZEE wa Mkoa wa Dar es Salaam, wamewasilisha kwa Rais Samia Suluhu Hassan matatizo manane wanayokumbana nayo katika uzee wao kubwa likiwa ni matibabu na uchumi.

Matatizo hayo yaliwasilishwa jana na Mwenyekiti wa Baraza la Wazee Mkoa wa Dar es Salaam, Salum Matimbwa, kwa niaba yao baada ya Rais Samia kukutana nao.

Akisoma risala yao, Mzee Matimwba alisema pamoja na nia njema ya kutoa huduma za matibabu kwa wazee, wamekuwa wakipata matatizo kadhaa kila wakienda kwenye matibabu.

"Hatupati baadhi ya vipimo na dawa tukifika hospitali, tunaomba tunapokwenda tupate vipimo vyote stahiki na dawa," alisema.

Pia alisema licha ya kuwapo kwa haki ya msamaha ya matibabu lakini matatizo mengine ni hawapati tiba za rufani na za kanda ikiwamo Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na kuomba wigo wa matibabu upanuliwe kwenye hospitali zote. "Sheria inayozungumzia wazee ipo sera iliyotungwa mwaka 2003, lakini tangu kipindi hicho hatujawahi kuwa na sheria inayozungumzia wazee, walemavu na watoto.

"Tunaomba hii sera ikamilike na itungwe iwe sheria ili kulinga haki na ustawi wa wazee, ikienda sambamba na sera ya taifa ya wazee," alisema.

Kuhusu fursa za kiuchumi, alisema wamekuwa wakikumbwa na matatizo mbalimbali na ili kujikwamua na kwa kuwa serikali inatoa mikopo kwa makundi maalum, wameomba nao waongezwe katika kundi la nne ili wanufaike.

Kadhalika, ameomba serikali upande wa Tanzania Bara iwafikirie wazee ili wapate pensheni kama inavyofanya serikali ya mapinduzi Zanzibar.

"Matatizo mengine tunayokumbana nayo ni kwenye usafiri wa vyombo vya umma, tunaomba vitengwe viti maalum vya kukaa wazee na vikimizwe kubeba wajukuu wetu wanapokwenda shule na kurudi nyumbani," alisema.

Kuhusu usimamizi na utekelezaji wa utawala bora, wazee hao walimwomba Rais Samia juhudi katika kushughulikia kero za wananchi na vyombo vya ulinzi na usalama kufanya kazi na kufuata sheria, kanuni, taratibu na miongozo waliyojiwekea na ikibidi jamii ishirikishwe.

Sambamba na hayo, waliomba uwakilishi wa wazee kwenye vyombo vya uamuzi kama ilivyo kwa viti maalum kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwenye mabaraza ya madiwani na Bunge ili wawe na watu wa kuwasemea. Suala lingine waliloliwasilisha kwa Rais ni ongezeko la wazee waliotelekezwa na jamii zao kutokana na sababu mbalimbali na kuomba serikali iboreshe makazi yaliyopo na kuyaongeza mengine ili watunzwe.

Naye Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, alisema jambo lolote linalohusu ustawi wa wazee katika nchi likimshinda Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, Naibu Waziri wa Afya na Waziri Mkuu, yeye yupo na atalitekeleza kwa nguvu zake zote.



Spika wa Bunge, Job Ndugai, akizungumza na viongozi kutoka Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS) walioongozwa na Rais wa chama hicho, Dk. Edward Hosea (kushoto kwake), walipomtembelea ofisini kwake, Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: BUNGE**

# Cheche za Samia kikao na wazee

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan, ameahidi katika kupanga safu ya kujenga uchumi wa nchi, akibainisha kuwa bila kujali chama, atachagua Mtanzania yeyote mwenye weledi, mahiri na anayeweza kuleta manufaa kwa taifa kwa kutumia uwezo alionao.

Vilevile, ameahidi kufanya mabadiliko yenye nia ya kutengeneza na siyo kubomoa.

Alitoa 'cheche' hizo jana mkoani Dar es Salaam alipozungumza na wazee wa mkoa huo na kubainisha kuwa Tanzania katika kujenga uchumi, kila Mtanzania anapaswa kuchangia bila kujali tofauti ya jinsia, rangi, kabila dini na imani ya siasa.

"Mathalani ni Mtanzania, imani yoyote ya siasa uliyonayo, dini yoyote uliyonayo, jinsia yoyote uliyonayo, lazima tuchangie katika kujenga uchumi wetu.

"Huko mbele katika kupanga safu za kujenga uchumi sitachagua...Mtanzania yeyote mwenye weledi, umahiri, anayeweza kuleta manufaa kwa taifa, nitamwingiza afanye kazi.

"Sitachagua katika chama kipi au yule katoka chama gani. Lengo ni kujenga umoja wa Watanzania na kila Mtanzania achangie kwa uwezo wake katika kujenga uchumi ili kuleta maendeleo ya wananchi," alisema.

Kuhusu mabadiliko, Rais Samia aliwaambia wazee hao kuwa wakiona yeye na wenzake wanayaleta katika nyanja mbalimbali, wajue wana nia njema ya kujenga nchi na siyo kubomoa.

"Katika mabadiliko haya yakikugusa, kijana wako akiguswa, ujue tunafanya kwa nia njema na siyo kubomoa, sote tutahisi fahari sana kama tutaitoa Tanzania ilipofikishwa na kuipeleka juu zaidi.

"Wote tutapangana kwenye safu ya kuleta maendeleo katika nchi, mradi ana tabia nzuri, hana dosari za maadili, hana dosari za kiusalama, anafaa kumtumia kuleta maendeleo ya nchi," alisema.

### SALAMU KWA WAHALIFU

Rais Samia pia alisema amesoma kwenye mitandao kuwa hali siyo nzuri Dar es Salaam kwa sababu uhalifu umerudi.

"Wanajaribu kina cha maji, ujambazi, upokonyaji umeanza kuja juu Dar es Salaam, ninaomba nitoe ujumbe wasijaribu kina cha maji, IGP (Mkuu wa Jeshi la Polisi) upo hapa, ninaomba ulishughulikie, na katika mitandao ile wamemtaja afande aliyekuwapo akakomesha wanasema mama turudishie, hali imeanza kuwa mbaya, Mkuu wa Jeshi, ninaomba hilo kaliangalie," alisema.

Rais Samia alisema hali ngumu haifanyi mtu kuwa jambazi na kuitaka jamii iwaangalie watoto wao wakue kwa kufuata maadili.

### KAMATI YA CORONA

Rais Samia alisema kamati aliyoiunda kushughulikia janga la corona, inaendelea vizuri na karibu itamkabidhi ripoti.

"Ninawaahidi yale yote yanayofanya wazee wawe kundi hatari, tunakwenda kuyashughulikia ili tuwakinge lakini pia tuwafundishe mbinu za kujikinga wenyewe dhidi ya maradhi haya," alisema.

Rais Samia alibainisha kuwa katika mkutano huo wa jana waliamua kuvaa barakoa kwa sababu wazee ndiyo kundi ambalo lipo kwenye hatari ya kupata maambukizi ya maradhi yaliyopo.

"Huwezi kujua nani anao, nani hana, sisi watoto wenu tunazunguka sana huko nchi nyingine, hatuwezi kujua, hivyo ni vyema kujikinga, mtuwie radhi ule uhuru wa kuvuta hewa umebanwa kidogo," alisema.

### ABEBA MATATIZO YAO

Rais Samia alisema matatizo waliyowasilishwa na wazee ambao takwimu zinaonyesha wapo milioni 2.6 nchini, ni ya msingi na serikali imeyapokea na itajitahidi kuyashughulikia na kueleza masuala yote yapo kwenye Ilani ya CCM na mpango wa miaka mitatu.

Kuhusu tiba, alisema ni haki yao ya msingi kuipata katika daraja lolote la hospitali kulingana na wanavyougua.

"Katika marekebisho ya sera tunayokwenda kuyafanya haya tutayatupia macho, shida ya kutanua wigo wa matibabu ninawaahidi tunakwenda kulifanyia kazi," aliahidi

Kuhusu ufumbuzi wa tiba ya wazee, alisema mbali ya sera, pia wanakwenda kutunga sheria, akikumbusha kuwa hata Ilani ya Chama Cha Mapunduzi (CCM) imeagiza kufanyia kazi suala la afya ya wazee.

"Mimi tayari nimeshaingia uzee, ninakuja kuwaunga huko, nisipoweka mambo vizuri nije kuyakute, sitakuwa na wa kumlilia, kwamba nafasi nimeitupa mwenyewe.

"Kuna hadithi sijui kama ni ya kweli, kulikuwa na Waziri wa Mambo ya Ndani Ghana, alichukua kiwango kikubwa cha fedha akakarabati jela.

"Bunge likamuuliza akasema 'heeh nikitoka hapa ni kule. Kwa hiyo ninatengeneza kabisa nikiingia nikute mazingira yawe mazuri'. Na mimi ninatengeneza kabisa ili nikija huko mambo yawe mazuri," alisema.

Kuhusu kuwezesha wazee kiuchumi, Rais alisema anakubaliana nao huku akiwaeleza kuwa wanafanya hivyo kwa kutumia Mfuko wa TASAF ambao kuanzia mwaka huu wanakwenda wilaya zote ili wale wenye sifa za kuingia kwenye mfumo huo wapate fursa.

Hata hivyo, alisema pamoja na kwamba TASAF inakwenda kumaliza mradi wake muda siyo mrefu, serikali inakwenda kuandaa mpango maalum wa kuwahudumia.

Rais Samia aliwaomba wazee wampe muda kuhusu pensheni za kila mwezi kuwa ataitolea uamuzi mbele ya safari kwa sababu hata wafanyakazi hawajapandishwa mishahara karibu miaka mitano.

Kuhusu makazi kwa wasiojiweza, Rais alisema siyo jambo analolipenda kwa sababu wazee walizaa watoto, hivyo jamii inatakiwa kuwatunza.

"Tuna kisingizio cha maisha magumu, kwangu ninaona ni maadili. Kweli maisha ni magumu, nitoe wito jamii ya Tanzania tutunze wazee wetu, shughuli za kuwaweka kwenye nyumba maalum inafanywa na wenzetu kule magharibi, sisi ni kutunza wazee wetu, wito kwa jamii tuendelee kuwatunza, pamoja na kwamba serikali itajenga makazi," alisema.

Kuhusu huduma kwenye vyombo vya usafiri wa umma, alisema nalo ni la maadili na kueleza kama mtoto amelelewa vizuri, anapomwona mzee amesimama kwenye basi, anapaswa kumpisha.

"Makondakta wanatakiwa kuhakikisha mzee amekaa kwenye kiti na kijana amesimama, utaratibu ukifanywa utazoeleka," aliagiza.

# UFAFANUZI

KATIKA toleo letu la Jumanne wiki hii, tulichapisha habari yenye kichwa cha habari kilichosomeka 'Utouh: Mikopo ya vyuo vikuu ifutwe'.

Kimsingi, habari hiyo ilihusu mahojiano ambayo Nipashe tulifanya na aliyekuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kuanzia mwaka 2006 hadi 2014, Ludovick Utouh, akishauri kutazamwa upya kwa mfumo wa bodi ya elimu ya juu ikiwamo kuangalia mbinu bora zaidi za urejeshaji mikopo kutoka kwa wanufaika badala ya kutegemea makato ya mishahara kwa kuwa wengi wao sasa wanahitimu na kukaa mitaani bila ajira.

Utouh pia alishauri kuwe na mkakati wa kukusanya Sh. bilioni 706.7 zilizoripotiwa na CAG wa sasa, Charles Kichere, kuwa ziko kwa wadaiwa sugu zaidi ya 128,000 ambao hawajulikani waliko.

Utouh pia alishauri kufutwa kwa madeni ya muda mrefu ambayo wanufaika hawajapatikana na siyo kufutwa kabisa kwa mikopo ya vyuo vikuu nchini.

Tunaomba radhi kwa usumbufu uliojitokeza.

**Mhariri**

## Mbaroni tuhuma kumuua mkewe kisa kutumia ARV

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga linamshikilia Peter Elias, mkazi wa Ndembezi Manispaa ya Shinyanga, kwa tuhuma za kumuua mke wake, Pili Luhende, kwa madai ya kutumia dawa za kupunguza makali ya Virusi vya Ukimwi (ARV) kwa kificho.


Kamanda Polisi mkoani Shinyanga, Debora Magiligimba, akitoa taarifa hiyo jana kwa vyombo vya habari, alisema tukio hilo lilitokea Mei 3, mwaka huu majira ya saa 10:30 usiku.

Alisema kuwa baada ya mtuhumiwa huyo kubaini mkewe anatumia dawa hizo kwa kificho, alimpiga na kusababisha kifo.

"Mtuhumiwa baada ya kutekeleza mauaji, aliuchukua mwili wa mke wake na kwenda kuutekeleza katika eneo la Mwagala darajani Mtaa wa Bugweto, Kata ya Ibadakuli," alisema Magiligimba.

Kamanda huyo alisema mwili wa marehemu umeshakabidhiwa kwa ndugu kwa ajili ya taratibu za mazishi na mtuhumiwa atafikishwa mahakamani upelelezi utakapokamilika ili achukuliwe hatua za kisheria.

Kamanda huyo alitoa wito kwa wanandoa kuacha tabia ya kujichukulia sheria mkononi badala yake wanapokuwa na migogoro, wapeleke malalamiko yao kwenye dawati la jinsia la Jeshi la Polisi au kwa maofisa wa ustawi wa jamii na kusuluhishwa.



Mhariri Mkuu wa Clouds Media Group, Joyce Shebe (kushoto), akipokea fomu kutoka kwa Mratibu wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Prisca Kabendera, jijini Dar es Salaam jana, kwa ajili ya kuwania nafasi ya Makamu Mwenyekiti wa Jukwaa hilo, katika uchaguzi mkuu wa viongozi wa TEF, unaotarajiwa kufanyika Mei 22, mwaka huu. Katikati ni Katibu wa jukwaa hilo, Neville Meena. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Vigogo TRC, Muhimbili wakalia kuti kavu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, ameziweka mtegoni bodi nane za mashirika ya umma kutokana na kutowasilisha taarifa za fedha kwenye ukaguzi uliofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka wa fedha 2019/20.

Kufuatia hali hiyo, Spika Ndugai ameagiza Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Hesabu za Serikali (PAC) kuuita uongozi wa menejimenti za mashirika hayo ikiwamo wenyeviti wao wa bodi ili kujieleza ni kwanini hawakufanya hivyo.

Spika Ndugai alitoa agizo hilo jana bungeni baada ya kipindi cha maswali na majibu kumalizika.

Aliyataja mashirika hayo kuwa ni Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Taasisi ya Mifupa (MOI), Shirika la Umeme (TANESCO), Soko la Bidhaa Tanzania (TMX), Mfuko wa Uwekezaji wa Pamoja (UTT), Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC), Shirika la Posta Tanzania na Shirika la Reli Tanzania (TRC).

Alisema mashirika hayo hayajafanyiwa ukaguzi kwa kigezo cha kutokuwa na taarifa na kutoa onyo kwa mengine.

"Kuna mashirika ambayo hayakuwa yameandaa hesabu zozote kwa maana ya CAG kuzikagua hesabu hizo kwa mwaka 2019/20. Kwa hiyo, hakuna taarifa ya CAG ya kupitia mashirika hayo inayokwenda kwenye Kamati ya PAC kutoka katika mashirika hayo.

"Ni uzembe wa hali ya juu kwa shirika kukosa hesabu zinazokagulika. Kwa hiyo, ninaagiza PAC kuyaita mashirika haya kwa ratiba mtakayojiwekea haraka sana ili yaje yajieleze ni kwanini hawakuwa kabisa na hesabu za kuweza kukaguliwa," aliagiza.

Alisisitiza uitwe uongozi wa menejimenti ikiwamo wenyeviti wao wa bodi na kama hawana sababu za maana, Bunge litashauri serikali bodi zao zivunjwe. "Kwa maajabu makubwa Shirika la Reli Tanzania, yapo mengine ambayo sijayataja.

"Kwa hiyo muwaite haraka hawa waje wajieleze maana hii ni hatari kabisa kwa mashirika makubwa kama haya yanakuwa shaghala baghala kiasi ambacho hawana hesabu zinazokagulika na CAG," alisema. Alitoa onyo kwa mashirika mengine yote kuwa wakati CAG akikagua hesabu zao baada ya Septemba, wawe tayari na hesabu zinazokagulika.

"Tunawalaumu sijui halmashauri na nani wenye mahesabu yenye hati chafu na zenye shaka wakati kuna mashirika makubwa hata hesabu hawana. "Sasa hilo haliwezekani kwenda namna hiyo. Kwa hiyo, PAC mfanye hii kazi na mtupe majibu ili tuweze kuishauri serikali," aliagiza.

# Watumishi 17,900 Mambo ya Ndani sasa kupandishwa vyeo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, amesema tayari moja ya idara za wizara hiyo, imepatiwa kibali cha kupandisha vyeo watumishi 17,900 na kwamba vigezo vitazingatiwa katika kufanya hivyo.

Akifungua kikao cha Baraza Kuu la Wafanyakazi wa Wizara hiyo jana jijini hapa, Waziri Simbachawene alisema wizara hiyo imeanza kupata maelekezo ya mambo waliyokuwa wanapigania wafanyakazi na kuwataka wachape kazi.

"Serikali inatambua changamoto na itaendelea kuzipunguza kabla ya muda unavyoruhusu, moja wapo ya idara kibali kimetoka cha kuwapandisha vyeo watu fulani fulani, siwataji hapa kama 17,900. Mchakato utaanza na tunaamini kibali kikubwa wengi watafurahi lakini watapanda kwa vigezo," alisema. Alisema upandishaji huo utazingatia vigezo vya ufanisi katika utendaji kazi.

Hata hivyo, alisisitiza mambo kadhaa kwa baraza hilo ikiwamo mwajiri na mfanyakazi kutambua kuwa sheria za kazi zimetungwa ili kuleta utulivu mahala pa kazi badala ya migogoro isiyo na tija.

Aidha, aliwataka kuzingatia kanuni za maadili ya utendaji kazi katika utumishi wa umma kuwa ni jambo la muhimu na kufanya kazi kwa bidii na uadilifu.

Simbachawene alisisitiza pia kwa vyama vya wafnayakazi kutumia vyombo vya ushauri ikiwemo baraza la wafanyakazi ili kutatua kero mbalimbali katika sehemu za kazi.

Waziri huyo alitoa wito kwa watumishi kuwa waadilifu na kuendelea kushirikiana na viongozi katika kutekeleza majukumu kwa bidii ili wizara ifike malengo yaliyopangwa pamoja na kuwezesha utekelezaji wa mipango ya kitaifa.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali Kuu na Afya (TUGHE) katika Wizara hiyo, John Jembele, alisema mkutano huo una lengo la kujadili mwenendo wa wizara kwa kuangalia wapi wamekwama.

"Mkutano huu unafanyika mara mbili kwa mwaka,na tunajadili bajeti yetu ambayo tayari imeshasomwa, tunaiangalia kwa ujumla namna inavyokwenda, na kikao kingine kitakachofuata tutafanya tathmini tumefanya nini katika bajeti tuliyopewa," alisema.

# Waziri abainisha fursa za biashara Kenya, Tanzania

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Kilimo, Profesa Adolf Mkenda amewataka wakulima na wafanyabiashara wa mahindi kuchangamkia soko la mahindi Kenya kwa kuwa tayari mipaka yote imeshafunguliwa.

Profesa Mkenda aliyasema hayo jana jijini hapa alipofungua mkutano wa wadau wa zao la muhogo kupitia chama cha zao hilo nchini (TAKAPA).

Alisema tayari Waziri wa Kilimo wa Kenya, Peter Munya, yuko mpakani Namanga kuhakikisha wanamaliza kero ya kibiashara baina ya nchi hizo.

Alisema viongozi baina ya nchi hizo wameshakutana na kumaliza mzozo wa kibiashara uliokuwa baina ya nchi hizo mbili, hivyo mipaka yote imefunguliwa.

"Leo (jana) Waziri wa Kilimo nchini Kenya amefanya kikao mpakani ambapo amezungumza na wafanyabiashara wa zao hilo la mahindi kuwaeleza ushirikiano wa kibiashara na kuweka sawa tofauti zilizokuwa zimejitokeza kwa namna moja ama nyingine.

"Zamani tulikuwa tunalima mazao kwa ajili ya kujikimu kwa chakula lakini hivi sasa tumeweka mkakati wa kulima kila zao kibiashara kwa kuyaongezea thamani, kulima kisasa ili yawe na tija kwa lengo la kuondokana na umaskini," alisema.

Kuhusu zao la muhogo, Profesa Mkenda alisema tayari Tanzania ilishatia saini mkataba wa kibiashara na China kwa ajili ya kupeleka Asia zao hilo la kibiashara.

Awali, Mwenyekiti wa chama hicho, Mwantumu Mahiza, alisema kilianzishwa mara tu baada ya Serikali ya Tanzania na China kutia saini mkataba wa makubaliano ya kibiashara kupitia zao hilo.

Mwantumu alisema kwa sasa wadau wa muhogo wanasafirisha bidhaa hiyo ya muhogo kupeleka China wakiwa wameiboresha na kuongeza thamani kwa kuikausha.



Mwenyekiti wa Taasisi ya Al- Hikma, Sheikh Nurdin Kishik (wa pili kushoto), akiwaongoza waumini na viongozi wa serikali, kushiriki futari iliyoandaliwa na taasisi hiyo, jijini Dar es Salaam juzi. Kulia ni Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Godwin Gondwe. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## SAKATA WABUNGE 19

# Spika Ndugai afunguka tena

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, ametolea ufafanuzi tena sakata la wabunge 19 wa Viti Maalum, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), akisema hawezi kuwafukuza hadi apate nakala za vikao vya chama hicho vilivyowafukuza uanachama.

Alitoa kauli hiyo bungeni jana akisisitiza kauli yake aliyoitoa mwanzoni mwa wiki kutokana na kuwapo kwa shinikizo la kuwafukuza wabunge hao bungeni.

Akizungumza jana baada ya kipindi cha maswali na majibu, Ndugai alisema ili atoe uamuzi kwa chama chochote cha siasa chenye nia ya kufukuza wabunge, ni lazima ajiridhishe kwa viambatanisho ambavyo ni katiba na muhtasari wa kuwafukuza kutoka kwenye chama husika.

"Nilitoa rulling (uamuzi) hapa ninaomba sasa nirudie tena maana wengine wanafikiri spika akiongea hapa ni masihara, spika anaoongoza Bunge kwa kufuata kanuni, katiba sheria, utaratibu, utamaduni na uamuzi wa maspika wengine.

"Uamuzi ninaotoa hapa ni uamuzi utakaotumika na hata watakaofuata baada yangu, rulling niliyotoa ninairudia, maana watu wanaweza kusema Ndugai hasa ni nani, suala siyo Ndugai, suala ni spika. "Ninarudia tena ili wanielewe vizuri maana hivyo ndivyo itakavyokuwa, hatulumbani, hapa sipo kwa sababu ya kulumbana na hii itatumika sasa na hata siku zijazo.

"Kwa vyama vyovyote vyenye kufukuza wabunge ambao ni wanachama wao, kwa kutumia dirisha la wanachama wao wanawafukuza watu ambao hao wanaofukuzwa ni wabunge," alisema.

Ndugai alisema wanapaswa wanapomwandikia Spika ni busara kumnakili Msajili wa Vyama vya Siasa.

"Lakini hata asipopeleka kule ni busara kufanya hivyo lazima barua hiyo iambatane na katiba yao, na muhtasari wa vikao vilivyohusika kuwafukuza wabunge hao," alisema.

Spika Ndugai alisema kama vyama vitafanya hivyo, vitamrahisishia kazi yake katika kutenda haki ili kuona kama ni kweli haki imetendeka kabla ya yeye kuweka baraka zake ili asionee watu kwa sababu ambazo hazina mbele wala nyuma.

"Sasa kama sina hivyo viambatanisho hivi, nitajuaje? Hiyo kamati kuu ndiyo kamati kuu ya chama fulani, anayejua ni Msajili sasa lazima nipate nakala zile niweze kuona ili niwaite na hao wabunge husika.

"Niwaambie jamani ninayo maandishi hapa yanayosema kuna hiki na hiki na hiki mnasemaje ili nao wajitetee mbele yangu niweze kutoa uamuzi, vinginevyo haiwezekani tu kwa sababu fulani anataka jambo fulani halafu ikawa, haiendi hivyo ni masuala ya haki." Alieleza masuala ya haki yanataka utaratibu na kwamba hilo litatumika kwa yeye na maspika wanaofuata hivyo viongozi wa vyama wanaoandika barua ya aina hiyo waambatanishe vitu hivyo na kwakuwa katiba hizi zinabadilika badilika aletewe katiba ambayo ndio inafanya kazi wakati huo.

"Kwa hiyo wale wenye nia hizo mnaogopa nini kuambatanisha hizo nakala za vikao vyenu? Kwa nini mnafichaficha, kuna nini ndani yake? Mbona ni jambo rahisi tu, mnaniletea mimi ninafanya kazi yangu wala haina shida," alisema.

# Uji wa chuma waua wafanyakazi kikatili

**Na Enock Charles**

WAFANYAKAZI wawili wamefariki dunia kwa kuunguzwa na uji wa chuma katika kiwanda cha kutengeneza bidhaa za chuma cha Fujian Hexingwang kilichoko Kijiji cha Kisemvule wilayani Mkuranga mkoani Pwani.

Kutokana na hali hiyo, Mkurugenzi wa Baraza la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Dk. Samuel Gwamaka, amezuru kiwandani huko na kukifunga kiwanda hicho hadi pale kitakaporekebisha miundombinu yake.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga, Steven Mwandambo, alisema juzi kuwa walipokea miili ya vijana wawili wakiwa tayari wamefariki dunia na kuwahifadhi katika hospitali ya wilaya hiyo kutokana na kuchomwa na uji huo.

Alibainisha kuwa wafanyakazi hao waliotambulika kwa majina Juma Pembe na Gerald Andrew, waliathiriwa na uji huo kuanzia katika kitovu hadi kifuani na kuongeza kuwa taarifa zaidi zitapatikana baada ya uchunguzi wa kitabibu.

"Tunao marehemu wawili ambao kimsingi walikuja wakiwa tayari wamekwishafariki dunia, hakuna tuliyemhudumia kwa kumtibu," alisema Mwandambo.

Kwa mujibu wa Dk. Gwamaka joto la kuyeyusha chuma ni sentigredi 1,400 hadi 1,500 ambayo ni zaidi ya mara 15 ya joto la mvuke wa kawaida, jambo ambalo ni hatarishi kwa mazingira ya wafanyakazi yasipowekewa mfumo mzuri wa kudhibiti kiwango cha joto kwa kuwekewa mfumo wa kulipooza.

"Tukio la leo ni matokeo ya watu kudharau uzingatiaji wa Sheria ya Mazingira na kuzingatia usalama wa mfanyakazi anapokuwa kazini.

"Hatuwezi kuendelea kupoteza maisha ya watu kwa kisingizio cha kuwekeza kiwanda.

"Kama ninyi hamna teknolojia, nendeni mkajifunze kwa wenzenu, kuna kiwanda cha Lodhia hapa jirani na kuna viwanda vingine kule Mikocheni, ninyi siyo kiwanda pekee," alisema.

Akisimulia jinsi tukio lilivyokuwa, Mkurugenzi wa kiwanda hicho, Xu Xingda, alisema baada ya uji wa chuma kumwagwa ili kuwekwa awamu nyingine, kiliwekwa aina ya chuma ambacho kina asili ya kulipuka na hivyo kusababisha mlipuko uliowarukia wahusika na kusababisha umauti kwao baada ya kuungua na uji huo na kutobolewa na vyuma.



Mpishi wa bia wa zamu wa kiwanda cha Serengeti Breweries Ltd (SBL) Mwanza, Christina Machaka, akitoa maelezo kuhusu bia inavyopikwa kwenye mitungi maalum kwa wanafunzi wa Chuo cha Kilimo Igabiro cha mkoani Kagera, walipotembelea kiwanda hicho, mwishoni mwa wiki, ikiwa ni sehemu ya kujifunza kwa vitendo kupitia wa programu ya Kilimo-Viwanda inayoendeshwa na kampuni hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Madai ya uongo yatikisa bima

**Na Mary Geofrey**

KAMPUNI ya Bima ya Sanlam imesema inapokea madai ya uongo kutoka kwa wateja wake kwa wastani wa asilimia 15 ya madai yote.

Imebainisha mbinu wanazotumia wenye madai ya uongo ni pamoja na kuwasilisha hati feki za vifo ilhali wahusika wapo hai na magari yaliyopata ajali kukatiwa bima kwa ajili ya kudai fidia.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Sanlam, Khamis Suleiman, alibainisha hayo jana mkoani Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari wakati wakitambulisha kaulimbiu yao mpya ya 'Ishi Kwa Kujiamini' yenye lengo la kujali maisha ya watu na mali zao.

Alisema vikwazo hivyo huvibaini na kuvitatua kupitia uchunguzi wanaofanya kabla ya kulipa fidia kwa hutumia wataalamu wao pamoja na vyombo vya dola.

"Tunakabiliwa na changamoto ya udanganyifu na tunapowabaini wahusika huwapa onyo kwa sababu tukisema tuwachukulie hatua za kisheria kama kuwapeleka mahakamani, tutawatisha wateja wetu wenye nia ya dhati," alisema Suleiman.

Alitaja kikwazo kingine ni kampuni za bima kushindwa kubadilishana taarifa kutokana na kutokuwa na mfumo huo.

Alisema kama wakifanikiwa kubadilishana taarifa, ni wazi watadhibiti uhalifu huo unaofanywa na wateja wasio waaminifu.

Ofisa huyo alisema kufuatia huduma wanayotoa kwa mstakabali wa Taifa na uchumi wa wananchi wake hulipa fidia za moto, mafuriko, wizi, ulemavu na vifo na kwa mwaka hutumia Sh. bilioni 40 kulipa fidia.

Alisema kwa mwaka wanalipa Sh. bilioni 12 serikalini kama kodi mbalimbali wanazotozwa.

Kampuni hiyo ina miaka 103 tangu kuanzishwa kwake Afrika Kusini ikiwa na biashara nchi 34 za Afrika.

# Mbaroni tuhuma wizi vifaa daraja la Kigongo - Busisi

**Na Richard Makore,** MWANZA

JESHI la Polisi mkoani Mwanza limewakamata watu wanane kwa tuhuma za kuhujumu miundombinu ya Daraja la Kigongo-Busisi linaloendelea kujengwa.

Inadaiwa watuhumiwa hao walikamatwa wakiwa na vifaa mbalimbali vikiwamo beam 19, bolt kubwa 16, waya na mashine ya kuchomelea vikiwa vimepakiwa katika gari aina ya Hiace.

Kamanda wa Polisi mkoani Mwanza, Jumanne Muliro, alisema baada ya mahojiano, watuhumiwa walisema walinunua vifaa hivyo kutoka kwa mafundi wa mradi huo.

Daraja hilo la kimkakati ambalo ujenzi wake ulianzishwa na Rais wa awamu ya tano Hayati Dk. John Maguli, mpaka kufikia mwanzoni mwaka huu, ujenzi wake ulikuwa umefikia asilimia 12. Kwa sasa daraja la muda katika ujenzi huo ambalo litatumika kupitisha vifaa vya ujenzi umekamilika.

Daraja hilo ambalo linaunganisha Wilaya za Misungwi na Sengerema mkoani Mwanza, linatarajiwa mwaka 2024 kwa gharama ya Sh. bilioni 700.

Kamanda Muliro aliwataka mafundi wa mradi huo kuacha tabia ya kuiba vifaa vya ujenzi vya mradi huo.

Katika tukio lingine, Kamanda Muliro alisema kuwa wilayani Misungwi, Ancelemi Musa (19) anadaiwa kuchomwa kisu na Alfred Emanuel aliyekuwa akimdai Sh. 15,000.

Katika tukio la tatu, Muliro alisema Pili Makuru (28), mkazi wa wilayani Ukerewe mkoani Mwanza, anadaiwa kumchoma kisu mgongoni, Getruda Mafolo na kisha na yeye kujichoma kisu ubavuni.

Kamanda Muliro alisema majeruhi wote wamelazwa hospitali wakiuguza majeraha.

Katika tukio lingine, Muliro alisema wilayani Magu mkoani Mwanza, Daud Musa (3) alivamiwa nyumbani kwao na kuliwa na fisi.

# Infinity, Letshego waungana fursa za mikopo ya ujenzi

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

INFINITY Real Estate Dodoma na Benki ya Letshego wamezindua huduma mpya ya mashirika hayo mawili kushirikiana kutoa mikopo ya ujenzi kwa wateja wake.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa huduma hiyo jijini Dodoma juzi, Meneja Biashara wa Infinity, Lulu Nzalalila, alisema ushirikiano huo utachangia wateja wengi kupata huduma za kitaalamu zaidi za ujenzi kwa bei nafuu.

"Watu wengi wanafikiri huduma za kitaalamu zinazotolewa na kampuni kama yetu ni ghali lakini siyo kweli kwani huduma hii tunayozindua leo inawalenga wateja wenye vipato mbalimbali ambao watashauriwa ipasavyo kuhusu mkopo huu," alisema wakati wa utilianaji saini kati ya Mkurugenzi Mtendaji wa Infinity Real Estate, Tumaini Mtei na Mkurugenzi wa Biashara wa Letshego, Dk. Goodluck Meena. Alisema baadhi ya huduma ambazo mikopo itatolewa ni pamoja na ujenzi wa nyumba kuanzia mwanzo, uendelezaji wa viwanja, umaliziaji wa ujenzi na ukarabati. "Watu wengi wana viwanja lakini hawana fedha za kuviendeleza au kufanya ujenzi. Tuna vifurushi mbalimbali kwa wateja wenye vipato mbalimbali ambapo pia marejesho yatakuwa na unafuu ili watu wengi zaidi waweze kutumia huduma hii ili wajenge na kumiliki nyumba," alisema.

Akatoa wito kwa Watanzania wajenge utamaduni wa kuomba mikopo ya nyumba, akisisitiza itasaidia kuongeza idadi ya wanaomiliki nyumba kama ilivyo katika nchi zingine.

"Kwa kupitia huduma hii tunataka kuunga mkono juhudi za serikali kuhakikisha Watanzania wengi zaidi wanamiliki nyumba na pia wanaweza kukopesheka katika benki na taasisi nyingine za kifedha, alisema huku akiwaasa Watanzania watumie huduma za kitaalamu ili kuhakikisha ubora.

Meneja Biashara wa Benki ya Letshego, Ruth Mpangala, alisema benki hiyo inafarajika kuwa sehemu ya ushirikiano huo na Infinity Real Estate Dodoma na kuwataka wateja watumie huduma hiyo ili wajipatie mikopo ya ujenzi. "Hii ni hatua nzuri mno na sisi Letshego tutahakikisha wateja wanapata huduma bora ikiwamo marejesho yenye unafuu kwa wateja wenye vipato mbalimbali ili kuhakikisha wakazi wengi zaidi wa Dodoma wanafaidika na huduma hiyo," alisema.

Alisema moja ya vigezo watakavyozingatia ni mteja mwenye kipato cha uhakika hata kama ni kidogo kwa kuwa kuna vifurushi mbalimbali kwa wateja na kuongeza kuwa wateja watatambulishwa kwa Benki ya Letshego na kampuni ya Infinity.

Infinity Real Estate Dodoma ilianza kutoa huduma miaka mitatu iliyopita na sasa ina wateja zaidi ya 300.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba, Yanga wapeni furaha mashabiki wenu

**HAKUNA** kulala! Hayo ni maneno kutoka kila upande wakati watani wa jadi, Simba na Yanga zote kutoka jijini Dar es Salaam zinazotarajiwa kukutana leo katika mechi ya marudiano ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Mchezo huo wa kiporo, unatarajiwa kuchezwa kuanzia saa 11:00 jioni na mwamuzi wa kati ametajwa kuwa ni Emmanuel Mwandembwa kutoka Arusha akisaidiwa na Hamdani Saidi wa Mtwara na Frank Komba wa Dar es Salaam huku mezani atakuwapo Ramadhan Kayoko wa hapa jijini.

Mbali na mechi hiyo ya watani kuwa na rekodi na matukio mbalimbali, lakini msimu huu ambao unaelekea ukingoni, itaendelea kutoa taswira za mbio za ubingwa ambazo bado ziko wazi kama ambavyo ni vigumu kusema moja kwa moja ni klabu zipi zitashuka daraja.

Simba ambao ni wenyeji wa mchezo huo na vinara katika msimamo wa ligi, wanahitaji kushinda ili kujiimarisha kileleni kwa kumwacha mbali mtani wake huku wakiwa wamecheza mechi pungufu.

Wekundu wa Msimbazi ambaye alilazimisha sare ya goli 1-1 katika mchezo wa kwanza, atahitaji kushinda ili kumaliza machungu ya kufungwa kwenye mechi ya fainali ya mashindano ya Kombe la Mapinduzi na hivyo kuondoa ubabe wa Yanga wa kupata matokeo chanya tangu mwaka huu ulipoingia.

Kwa upande wa Yanga, wao watashuka dimbani wakihitaji pointi tatu muhimu kwa ajili ya kumpa presha mtani wake ambaye anaamini na anatamba amejiandaa kutwaa ubingwa kwa mara ya nne mfululizo, na yeye akijipanga kuharibu mikakati hiyo.

Yanga inaamini endapo itashinda katika mchezo wa leo, itakuwa imewapa furaha mashabiki na wanachama wake, lakini itarejea kwenye mbio za kuwania taji hilo linalotoa tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika na kukataa mbeleko ya kubebwa na hasimu wao.

Kwa maana hiyo, mbali na kuondoka na pointi tatu, mechi ya leo imekuwa ikizungukwa na malengo mengine ambayo yote yanaongeza kuufanya mchezo huo kuwa na ushindani na ugumu kwa kila upande. Ni muhimu mbali na matokeo ya ushindi, mechi hiyo ni moja ya michezo inayotazamwa na idadi kubwa ya mashabiki, hivyo kila anayehusika anatakiwa kuonyesha ubora wake wa hali ya juu ili kujiweka sokoni.

Kama kuna mchezaji ataonyesha kiwango bora, nidhamu na ufundi, ni wazi atakuwa amewavutia mawakala ambao wanatafuta wachezaji wa kuwapeleka Ulaya huku makocha pia wakizipandisha 'CV' zao na hatimaye wanaweza kupata ofa mpya zitakazokuwa na maslahi bora zaidi. Lakini ili mambo yote yaonekane, kila upande unatakiwa kufanya vyema majukumu yake na hapo matunda mazuri yatapatikana badala ya kusaka mchawi pale matokeo chanya yatakapokosekana.

Wachezaji kumbukeni mechi hii ya 'dabi' mbali na kuisogeza timu yako katika 'harufu' ya kutwaa ubingwa wa msimu huu wa 2020/21, pia hutoa nafasi kwa nyota kujiweka sokoni kuelekea msimu mpya kwa kuboresha mikataba kwa wale ambao bado mikataba yao haijamalizika au kuzivutia timu nyingine kukusajili.


Ni vyema wachezaji na waamuzi kuingalia dabi hii kama fursa ya kutimiza ndoto zao kwa sababu tunaamini hakuna mchezaji, mwamuzi au kocha asiyependa kuona anasonga mbele katika majukumu ambayo anayafanyia kazi kila siku.

Ifike wakati wachezaji na waamuzi wakautendea haki 'ukubwa' wa mchezo huu kwa kuonyesha viwango bora, nidhamu na bila kusahau mashabiki kujua mwisho wa mipaka yao ili kuifanya mechi hiyo kubwa nchini kumalizika kwa salama na utulivu.

Nipashe inawatakia kila la kheri wahusika wote muhimu katika mchezo wa leo kwa sababu inaamini mechi hii ni moja ya michezo inayoonyesha taswira ya soka la Tanzania na ubora wa Ligi Kuu Bara.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Barnabas Maro

## Muungwana Lazima Nilonge

# Halahala Simba na Yanga

**WAHENGA** walisema, "Maneno ni daraja, hayazuii maji kuteremka." Maana yake daraja haliwezi kuyazuia maji ya mto yasiteremke. Aidha maneno nayo hayawezi kumzuia mtu kufanya jambo aliloazimia (dhamiria.)

Methali hii inatumiwa kumnasihi mtu aliyeazimia kufanya jambo fulani asikate tamaa au asivunjwe moyo na maneno ya watu ambayo hayamdhuru kwa namna yoyote. Huweza pia kutumiwa na mtu aliyeazimia kufanya jambo fulani kujitetea dhidi ya maneno ya binadamu.

Kabla ya mechi ya leo Jumamosi kati ya Simba na Yanga, kumekuwa na maneno mengi, hasa kwa mashabiki wa Simba kuibeza (kitendo cha kupuuza kitu, mtu au jambo; kitendo cha kuonyesha hisia ya kejeli kwa mtu; dharau, tweza) Yanga.

Hakuna ubishi kuwa Simba ya msimu huu iko vizuri kwa kila hali - kimchezo, kifedha na ushangiliaji wenye mbwembwe (mikogo) za kila aina. Yote hayo yanaipa Simba ushindi dhidi ya Yanga ingawa mara nyingi timu inayoonekana kuwa bora zaidi ya nyingine ndiyo hupoteza mchezo!

Pamoja na yote hayo, mara nyingi timu ianyoonekana kuwa bora ndio inayoshindwa au kwenda sare na timu isiyopewa nafasi ya ushindi!

Kihistoria Yanga ndiyo iliyoshinda mara nyingi zaidi tangu mwaka 1965 mpaka sasa. Yanga na Simba zimepambana mara 105, Yanga ikishinda mara 37 dhidi ya Simba iliyoshinda mara 31 na sare mara 37 kila moja.

Kadhalika kwa kipindi hicho chote, Yanga imepoteza mechi 31 ilihali Simba ikipoteza mara 37. Kwa kipindi hicho Yanga ilipata alama 148 na Simba kupata alama 130 kwa matokeo haya, hapana shaka ndio sababu ya Yanga kuitwa "mabingwa wa kihistoria."

**Kadhalika kwa kipindi hicho chote, Yanga imepoteza mechi 31 ilihali Simba ikipoteza mara 37. Kwa kipindi hicho Yanga ilipata alama 148 na Simba kupata alama 130 kwa matokeo haya, hapana shaka ndio sababu ya Yanga kuitwa "mabingwa wa kihistoria."**

Kwa miaka mitatu mfululizo, Simba imetwaa taji Ligi Kuu huku Yanga ikisuasua, yaani kusitasita katika kufanya jambo.

Ilivyo sasa kila upande unatoa maneno ya majivuno kwa timu yao dhidi ya upande mwingine. Kumekuwa na maneno ya pande zote mbili kutoa vitisho dhidi ya upande mwingine kuhusu mechi ya leo Jumamosi.

Gazeti maarufu la michezo nchini limekuwa likiandika maneno ya kejeli yatolewayo na wachezaji na wapenzi wa timu zote mbili. Maneno mengine ni ya kuikatisha tamaa Yanga huku wanaosemwa kwa vitisho wakisema: "Nyie... jidanganyeni." Nakuachia wewe msomaji utambue ni upande gani uliosema maneno hayo.

Kwa yote hayo, nakumbuka wahenga walivyosema kwamba: "Mwenye kelele hana neno." Kwamba aghalabu mtu anayepiga kelele huwa hana madhara yoyote. Methali hii hutumiwa kutukumbusha kuwa hatupaswi kumwogopa mtu mwenye kelele au fujo kwa kuwa kwa kawaida hana neno.

Nawakumbusha mashabiki na wapenzi wa timu za Simba na Yanga ambao ndio wenye maneno machafu yanayokera, kuwa "Asiyekiri ushindi hakuwa mshindani." Maana yake mtu asiyekubali baada ya kushindwa si mshindani. Hutumiwa kuwanasihi binadamu kukubali wakishindwa au kukiri udhaifu wao.

Kwa upande mwingine, "Bendera ipepeayo sana mwishowe huchanika." Maana yake bendera au beramu inayopepea sana mwishowe huchanika. Hutumiwa kumpigia mfano mtu anayejisifu na kujitangaza kwa uwezo alionao. Hatimaye uwezo huo utaisha na abakie katika hali duni au mbaya.

Halahala Yanga na Simba kwani "Ajidhaniye amesimama anapaswa kuangalia asianguke." Methali hii yatufunza tusiwe na kiburi. Inawakanya wenye vyeo wajichunge kwa kuwa wanaweza kuharibikiwa na kuwa si chochote. Tunaomba mchezo mzuri na atakayefungwa akubali kushindwa tena itakuwa uungwana kupeana mikono kwa washindwa kuwapongeza washindi. Huo ndio uungwana.

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**

# Serikali yaja na sera ya tija

SERIKALI iko katika mpango wa kuandaa sera ya taifa ya tija na ubunifu ambayo itaweka mfumo thabiti wa kupima tija na ubunifu katika ngazi ya taasisi, sekta na taifa kwa lengo la kutekeleza miradi mikubwa kwa ufanisi.

Mpango huu unatokana na mchakato wa serikali wa kutekeleza mipango sita ili kuhakikisha utekelezaji wa miradi mikubwa nchini unakuwa na tija na kuwanufaisha Watanzania.

Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Ajira, Kazi na Vijana, Patrobas Katambi, alisema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Dk. Alice Kaijage.

Mbunge huyo alihoji serikali ina mpango gani wa kukitumia kikamilifu kitengo cha kukuza tija kilichoko Ofisi ya Waziri Mkuu ili kuhakikisha utekelezaji wa miradi mikubwa nchini unakuwa wa tija na kuwanufaisha Watanzania.

Akijibu swali hilo, Katambi alisema katika kuhakikisha kitengo hicho kinatekeleza majukumu yake kikamilifu, serikali imepanga kutekeleza mipango sita ikiwamo kuandaa sera ya taifa ya tija na ubunifu ambayo itaweka mfumo thabiti wa kupima tija na ubunifu.

"Mpango huu unahusu pia kufanya utafiti wa tija katika viwanda vya mfano vilivyoko mikoa ya Dar es Salaam na Pwani, kuandaa na kuwezesha wiki ya tija na ubunifu, kuandaa na kuwezesha Mpango wa Kitaifa wa Tuzo za Tija na Ubunifu na kuendesha programu 24 za kuwajengea uwezo wadau juu ya dhana, kanuni na viwango vipya vinavyotokea katika tija, ubunifu na ufanisi wa viwanda," alisema.

Katambi alisema serikali kupitia Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano wa Tatu (FYDP III) imeelekeza sekta binafsi kushiriki katika miradi mikubwa ya kitaifa kwa kushirikiana na taasisi zingine kikiwamo Kitengo cha Ukuzaji tija.

Alisema lengo la kufanya hivyo ni kuboresha ufahamu wa sekta binafsi juu ya masuala ya ufanisi, ushindani na utoaji wa huduma bora kwa jamii.



Waziri wa Maji, Jumaa Aweso (kushoto), akijadiliana jambo na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wafamasia kuajiriwa kupunguza pengo

KATIKA mwaka wa fedha 2021/22, serikali itaajiri watumishi 10,467 wa sekta mbalimbali wakiwamo wafamasia ili kukabiliana na uhaba wa wataalamu uliopo nchini, Bunge limeelezwa.

Hayo yalisemwa jana na Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Festo Dugange, alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Bukene (CCM), Selemani Zedi.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji kama serikali haioni umuhimu wa kuajiri wafamasia angalau katika kila kituo cha afya nchini ili kuimarisha usimamizi wa mtiririko wa upatikanaji dawa.

Akijibu swali hilo, Dk. Dugange alisema kwa mujibu wa Ikama, mfamasia anapaswa kuwepo katika ngazi ya hospitali.

Hata hivyo, alisema kwenye ngazi ya vituo vya afya na zahanati, ikama inaelekeza kuwapo kwa mteknolojia ya dawa au mteknolojia msaidizi wa dawa.

"Kada hizi ni muhimu kuwapo kwenye vituo vya kutolea huduma za afya ili kuimarisha uratibu na usimamizi wa bidhaa za afya. Kuanzia Mei 2017 hadi Februari 2021, Ofisi ya Rais-TAMISEMI imeajiri wafamasia 79, wateknolojia wa dawa 313 na wateknolojia wasaidizi wa dawa 160," alisema.

Katika kuhakikisha wataalamu hao wanakuwapo, alisema watumishi wa kada mbalimbali watakaoajiriwa mwaka 2021/22 watasambazwa kwenye halmashauri zote nchini.

Katika swali la nyongeza, mbunge huyo alihoji kama serikali haioni umuhimu wa kuruhusu waganga wa wilaya na wakurugenzi wa halmashauri zenye uwezo wa kuajiri wataalamu hao kwa mkataba wakati wanasubiri ajira.

Akijibu swali hilo, Dk. Dugange alisema serikali inafahamu kuna upungufu wa wataalam wa teknolojia ya dawa lakini pia wateknolojia wasaidizi wa dawa.

"Kweli kama mbunge alivyoelezea tunahitaji kuwa na wataalamu hawa ili kuhakikisha vituo vyetu vinaweka matokeo mazuri ya dawa lakini uagizaji kulingana na utaalam ili kuhakikisha dawa zinapatikana katika vituo vyetu," alisema.

Alimhakikishia kuwa serikali ilishatoa maelekezo kwa wakurugenzi ambao halmashauri zina uwezo wa mapato ya ndani, kuajiri kwa mikataba wataalamu hao.

"Nimhakikishie kuwa jambo hili limeshafanyiwa kazi na serikali na nitoe wito kwa wakurugenzi wote wa mamlaka za serikali za mitaa nchini kutumia fursa hiyo kwa wale wenye uwezo wa kuajiri ili kutumia fursa hiyo ya kuajiri," alisema.




**Habari zote na Augusta Njoji, DODOMA**

## Mikakati yawekwa kufanya Kiswahili bidhaa kimataifa

WIZARA ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo imeanzisha mipango kadhaa ya kimkakati ya kukifanya Kiswahili kuwa bidhaa ya kimataifa na tayari wataalamu 1,308 wamesajiliwa kwenye kanzidata.

Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Pauline Gekul, alibainisha hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Singida Mjini (CCM), Mussa Sima.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji serikali ina mpango gani wa kuifanya lugha ya Kiswahili kuwa bidhaa ya kimataifa ili kuendeleza na kukuza utamaduni wa Watanzania duniani.

Gekul alisema serikali pamoja na mipango hiyo, pia serikali imenunua vifaa vya kisasa vya mafunzo ya ukalimani kwa vitendo na matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) katika ukuzaji wa Kiswahili.

"Tayari tunao mpango wa kufundisha Kiswahili kwa wageni kupitia balozi zetu nje ya nchi. Vilevile, serikali imeboresha na kuimarisha mafunzo ya stadi za kufundisha Kiswahili kwa wageni," alisema.

Pia alisema pamoja na kutoa machapisho ya Kiswahili rahisi kwa wataalamu kadhalika kwa lengo la kusaidia nchi zilizoonyesha nia ya kuingiza Kiswahili katika mitaala yao ya elimu mfano Afrika Kusini, Namibia, Rwanda na Uganda.

"Wakati wa mkutano wa 39 wa wakuu na viongozi wa serikali wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), serikali ilifanikiwa kukifanya Kiswahili kuwa moja ya lugha nne rasmi zinazotumiwa wakati wa vikao na mikutano ya nchi hizo," alisema.

# Waliokosa umeme waondolewa hofu

**Na Mwandishi Wetu**

MKURUGENZI Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Mhandisi Amos Maganga, amewataka wakazi wa vijijini ambao maeneo yao hayakufikishiwa umeme baada ya miundombinu yake kufikishwa, kuondoa hofu kwa kuwa watapelekewa kupitia mradi wa ujazilizi ambao umeshaanza kutekelezwa.

Maganga alitoa ufafanuzi huo wakati akizungumza kupitia Kipindi cha Sema Kweli kilichorushwa na Kituo cha Runinga cha Channel Ten, juzi.

Alisema serikali ilibuni mradi wa ujazilizi ili kwenda kujazia maeneo ambayo yamefikiwa na miundombinu ya umeme lakini haijasambaa eneo zima ili kuhakikisha wananchi wote wanapata huduma hiyo muhimu.

"Sasa hivi ukienda vijijini, utakuta malalamiko ya baadhi ya wananchi kuwa umeme umefika kwenye kijiji lakini umepelekwa katika taasisi kadhaa kama vile shule na zahanati huku maeneo mengine yakirukwa.

Jambo la msingi ni kuwa tumekwishafikisha miundombinu ambayo ni gharama zaidi kuiweka. Sasa tunatekeleza miradi ya kujazia umeme vitongoji vyote, hivyo wananchi wasiwe na wasiwasi," alisisitiza.

Kuhusu kupeleka umeme katika visiwa, Mhandisi Maganga alisema serikali kupitia REA inaendelea kuvipelekea umeme visiwa vyote nchini kwa kutumia teknolojia mbalimbali zikiwamo za umeme jua na upepo.

Alisema visiwa 72 hadi sasa vimekwishapelekewa umeme kati ya 196 vilivyopo nchini na kwamba mpango unaoendelea kutekelezwa ni kuviunganishia umeme visiwa vingine takribani 53 ambavyo vina makazi ya kudumu ya watu.

"Visiwa 36 kati ya 53 vitaanza kupelekewa umeme kuanzia Julai, mwaka huu, na vitakavyosalia vitapelekewa katika bajeti ijayo," alisema.

Akizungumzia sekta ya umeme vijijini ilivyonufaika na Mpango wa Serikali wa Uchumi wa Viwanda, alisema uhamasishaji huo wa serikali umechochea wananchi wengi kuanzisha viwanda vinavyotengeneza vifaa mbalimbali vya umeme hivyo kuwezesha upatikanaji wake hapa nchini.

# Waziri ataka makandarasi kurejesha mikopo

**Na Joseph Mwendapole,** ARUSHA

SERIKALI imewataka makandarasi wanaokopeshwa na Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB), kulipa kwa wakati mikopo wanayopata ili makandarasi wengine wanufaike na fursa hiyo.

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mwita Waitara, alitoa agizo hilo jana jijini hapa wakati wa hafla ya kufunga mkutano wa mashauriano baina ya bodi hiyo na makandarasi wazalendo.

CRB ilianzisha mfuko wa kusaidia makandarasi wa ndani uitwao (Contractors Assistance Fund- CAF), ambapo makandarasi wote bila kujali madaraja yao, wanaweza kukopeshwa hadi Sh. milioni 100 kwa ajili ya kutekeleza miradi.

Naibu Waziri aliipongeza bodi kwa kuanzisha mfuko huo ambao alisema iwapo utatumika vizuri, utakuwa msaada mkubwa kwa makandarasi wa ndani kukuza mitaji yao.

Alisema inashangaza kuona baadhi ya makandarasi wanaanza mizengwe wanapokopeshwa fedha hizo hali ambayo inaweza kusababisha mfuko kufa.

"Ndugu zangu mnapoaminiwa lazima na ninyi mwaminike, lazima mheshimu makubaliano mliyotia saini wakati mnachukua hizo fedha. Wengine badala ya kulipa wanakimbilia mahakamani lakini sitarajii mtakuwa hivyo," alisema.

Kuhusu ujenzi wa miradi mikubwa, Naibu Waziri alisema serikali itaendelea kutenga miradi ya ujenzi maalum kwa ajili ya kufanywa na makandarasi wazalendo lakini kinachotakiwa kwao ni uaminifu na uzalendo kwa nchi yao.

"Mkandarasi unapopewa mradi wa nchi yako, fedha za nchi yako, mradi utanufaisha wananchi wenzako. Kwa nini sasa ufanye ovyo ovyo na kusababisha hasara kubwa kwa serikali? Lazima uwe na uchungu na nchi yako," alisema Waitara.

Aliipongeza CRB kwa kuandaa mikutano ya kuendelea kuwajengea uwezo makandarasi wa ndani ili wawe na uwezo wa kutekeleza miradi mikubwa kama kampuni za nje hali itakayookoa fedha nyingi za umma.

Pia alishauri mikutano kama hiyo iendelee kufanyika mara kwa mara kwa sababu inawezesha kupata mrejesho kuhusu matatizo ya makandarasi na kuyatafutia ufumbuzi ili kukua na kusonga mbele.

Waitara aliitaka CRB kuendelea kufuatilia na kukagua miradi inayofanywa na makandarasi wazalendo ili kuwasisitiza kuimaliza kwa wakati na kwa ubora unaotakiwa na hatimaye waendelee kuaminika.

"Nimefurahi kusikia kwamba hivi karibuni mtafuatilia miradi. Nendeni mkakague na ule wa Kilosa mzungumze nao waumaliza kwa wakati kwa sababu wakifanya vizuri watakuwa wamewatengenezea fursa wenzao. Wakishindwa watawaangusha maana hawataaminika," alisisitiza.

Msajili wa CRB, Rhoben Nkori, alimweleza Naibu Waziri kuwa hivi karibuni watatembelea miradi inayofanywa na makandarasi iliyotengwa kwa ajili ya kuwajengea uwezo ili kujua kero zao na kutafuta ufumbuzi.

Alisema bodi hiyo itaangalia matatizo ya makandarasi wa ndani inayosababisha serikali kutekeleza miradi yake kwa kutumia mafundi wake kupitia utaratibu wa force account.



Naibu Waziri Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deogratius Ndejembi (kulia), akipokea taa inayotumia nishati ya jua kutoka kwa Meneja Mauzo kampuni ya D. Light, Kanda ya Kati, Noel Maktauwa, baada ya kuzindua duka la kampuni hiyo, katika Barabara ya Nyerere, jijini Dodoma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# DC afichua chanzo ukosefu wa ajira kwa vijana katika viwanda

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKUU wa Wilaya ya Kibaha, Mhandisi Martine Ntemo, amesema pamoja na kuwapo kwa idadi kubwa ya viwanda katika wilaya hiyo, bado kuna kikwazo cha vijana kukosa ajira baadhi ya sababu zikielezwa kuwa ni ujira mdogo.

Mbali na ujira pia inaelezwa kuwa wapo waajiri ambao hawatimizi mikataba ya kazi ikiwamo kutowapatia wafanyakazi vitendea kazi vinavyotakiwa wawapo kiwandani.

Kutokana na hali hiyo, Ntemo amesema jana kuwa wanafuatilia kwa undani vikwazo hivyo ili viondolewe na vijana washawishike kuomba kazi kwenye viwanda vilivyopo.

Mtemo alisema hayo juzi alipokuwa kwenye mkutano na wananchi wa Kata ya Msangani uliolenga kusikiliza kero na kujadiliana namna ya kuzitatua akiwa ameambatana na wakuu wa taasisi mbalimbali zikiwamo za umeme, maji na barabara. Aidha, Ntemo aliwataka wananchi kuhakikisha wanatafuta umiliki halali wa maeneo yao pamoja na kuunganisha nguvu kuhifadhi misitu iliyopo karibu na maeneo yao.

Katika kikao hicho, baadhi ya wananchi waliopewa maeneo ya kulima katika shamba la miti Ruvu Kaskazini, waliomba kumilikishwa kwa kuwa wamekuwa wakilima kwa zaidi ya miaka 20 sasa.

Akizungumza kwa niaba ya zaidi ya wakazi 300 wanaolima katika shamba hilo, Mohamed Mtukula, alimwomba mkuu wa wilaya kusimamia suala hilo ili wajenge na kufanya maendeleo kwenye maeneo hayo.

Mhifadhi Mkuu wa Shamba hilo, Fortunata Senya, alisema familia 319 ambazo zinalima katika shamba hilo, ziliingia mkataba wa miaka 10 na kila familia ilipata ekari 7.5 na ilitakiwa wawe wamesimamisha shughuli za kilimo baada ya mkataba kumalizika.

Senya alisema shamba hilo haliwezi kumilikishwa kwa wananchi litaendelea kubaki kuwa hifadhi na kwamba familia hizo zinatakiwa kuendelea kuzingatia masharti ya mkataba ambao ni kulima mazao ya muda na kupanda miti.

"Nilitegemea leo (juzi) hapa wananchi tuliowapa kulima kwenye shamba hilo watoe shukrani na si kuilaumu serikali kama walivyofanya leo. Hapa mnaomba mmilikishwe wakati hata hizo ekari 7.5 mlizopewa kila familia hakuna aliyelima zote.

"Wengine wamelima ekari tatu, mbili hadi moja kati ya hizo 7.5 na kusababisha mapori kuendelea kwenye shamba. Ninachotaka kuwaambia shamba hili haligawiwi litaendelea kubaki kuwa eneo la hifadhi," alisema. Mhifadhi huyo alisisitiza kuzingatiwa masharti ya mkataba walioingia wananchi hao na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) katika shamba hilo.



# TEA kumaliza adha madarasa, matundu ya vyoo jijini Dodoma

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAMLAKA ya Elimu Tanzania (TEA), imejipanga kutekeleza mradi ya ujenzi wa madarasa na matundu ya vyoo kwa shule za msingi nne jijini Dodoma.

Akitoa maelezo ya awali kuhusu mradi huo jana, Mkurugenzi Mkuu wa TEA, Bahati Geuzye, alisema kazi hiyo itagharimu Sh. bilioni 1.9 na utatekelezwa katika shule za msingi Kisasa, Medeli, Kizota na Mlimwa C.

Alisema mradi huo umelenga katika kutatua kero ya madarasa ya kusomea na matundu ya vyoo katika shule hizo.

Gauzye aliwataka wadau wote wahusika wa usimamizi wa mradi huo kuhakikisha kazi yote inakamilika ndani ya miezi minne ili kuwapa fursa wanafunzi kuanza kutumia miundombinu hiyo kwa wakati.

Kwa upande wake, Mbunge wa Dodoma Mjini, Anthony Mavunde, alishukuru serikali kupitia TEA kwa kuwapatia fedha hizo.

"Ninaishukuru serikali chini ya Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutupatia fedha za ukarabati na ujenzi wa matundu ya vyoo ambazo kwa kiasi kikubwa zitapunguza adha kwa wanafunzi wetu wa shule za msingi," alisema.

Alibainisha kuwa mradi huo umekuja wakati wa mwafaka hasa ikizingatiwa kwamba kwa sasa mahitaji ya vyumba vya kusomea kwa wanafunzi ni makubwa sana hali inayosababishwa na mwitikio wa sera ya elimu bure na kuhamia kwa serikali jijini Dodoma.

"Natoa rai kwa kamati za shule kuhakikisha wanasimamia ipasavyo fedha za mradi huu kwa uaminifu na uadilifu mkubwa ili matokeo ya mwisho ya lengo lililokusudiwa yaonekane," alisema.

Naye Mstahiki Meya Prof. Davis Mwamfupe, alishukuru serikali kupitia TEA kwa mradi huu mkubwa na kuahidi kuendelea kutenga bajeti kubwa ya elimu kwenye miradi ya maendeleo ili kupunguza matatizo ya sekta ya elimu.




Meneja wa Tigo Kanda ya Kaskazini, Said Idd (katikati), akifafanua jambo kwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Ndalichako, kuhusu huduma zinazotolewa kampuni hiyo, wakati wa maonyesho ya Wiki ya Ubunifu kuelekea Kilele cha Mashindano ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU) 2021, katika Uwanja wa Jamhuri, jijini Dodoma jana. Kushoto ni Mtaalamu wa Mauzo wa Tigo Biashara, Joachim Chuwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TAMISEMI yaweka utaratibu wa uhamisho

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KATIBU Mkuu Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Prof. Riziki Shemdoe, amesema uhamisho wa watumishi wa Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa utafanyika mara nne.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi, Prof. Shemdoe alisema kila tarehe 10 ya mwezi unaofuata baada ya robo mwaka kwisha, uhamisho utafanyika na majina yatawekwa kwenye tovuti ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI.

"Robo kwanza ya mwaka yaani Julai - Septemba majina ya uhamisho yatakuwa yanatoka tarehe 10 Oktoba, na robo ya Pili Oktoba - Desemba majina ya uhamisho yatatoka Januari 10.

"Katika robo ya tatu ya Januari-Machi majina ya uhamisho yatatoka Aprili 10 na robo ya mwisho ya Aprili-Juni majina ya uhamisho yatatoka Julai 10," alisema.

Aidha, Prof. Shemdoe alibainisha kuwa majina ya watumishi wote watakaohamishwa yatawekwa kwenye tovuti ya Ofisi ya Rais TAMISEMI ambayo ni www.tamisemi.go.tz.

Pia aliwataka Makatibu Tawala wa Mikoa yote nchini kuwasilisha orodha ya watumishi wa kuhama ofisi ya Rais-TAMISEMI kila tarehe 5 ya mwezi unaofuata baada ya robo mwaka.

Aidha, alisisitiza makatibu tawala wote kutokupitisha maombi ya watumishi wanaotaka kuhamia kwenye majiji, manispaa na miji kwa kuwa maeneo hayo yana idadi kubwa ya watumishi.

Hata hivyo, Prof. Shemdoe aliwataka makatibu tawala kuwapa kipaumbele watumishi wenye matatizo mbalimbali yaliyothibitishwa.

Pia aliwataka watumishi wote kubaki kwenye vituo vyao na barua za uhamisho zitatumwa kwa waajiri wao na wataona majina yao kwenye tovuti ya ofisi hiyo.

Alisema barua za uhamisho za kipindi cha nyuma ambazo zilishafika Ofisi ya Rais, TAMISEMI zinashughulikiwa na majina yatatolewa kila mwezi mpaka Juni 30 kabla utaratibu mpya haujaanza kutumika.

# Bosi apigia debe umeme wa REA

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KAIMU Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA) Mhandisi Jonas Olotu, amewataka wananchi kuchangamkia fursa ya kuunganishiwa umeme ili kuanzisha miradi mbalimbali itakayo wasaidia kujiinua kiuchumi.

Olotu aliyasema hayo jana jijini Dodoma alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari katika kikao baina ya REA na timu ya wafadhili wa miradi iliyo chini ya wakala.

Alisema wananchi wanatakiwa kutumia fursa iliyopo hivi sasa ya upatikanaji wa nishati hiyo hasa katika maeneo ya vijijini.

Kwa mujibu wa Olotu, mwitikio wa wananchi katika kuunganishiwa umeme kwenye maeneo ya vijijini bado uko chini, hivyo kuna haja ya kuhamasisha wananchi kupata huduma hiyo.

"Wananchi wanatakiwa kuchangamkia fursa hii ya kuunganishiwa umeme kwani hivi sasa gharama za kuunganisha ni Sh. 27,000 na kwa wale ambao hawajaweka mfumo wa umeme katika nyumba, wanaweza kutumia kifaa cha umeme tayati (Umeta)," alisema Olotu.

Alisema katika miradi ya REA wanataka kila mwananchi katika maeneo ya vijijini kuunganishiwa huduma hiyo.

"Hatutaki kumwacha mtu tunataka kila tunapomaliza miradi katika eneo moja kila mtu anakuwa ameunganishwa na huduma hii ya umeme," alisema.

Mwenyekiti wa Bodi ya REA, Mhandisi Julius Bundala, alisema wanatarajia hadi ifikapo Desemba 2022, vijiji vyote nchini kuwa vimefikiwa na huduma ya umeme.

Bundala alisema katika kipindi cha mwaka 2015, vijiji 2,018 ndivyo vilikuwa vimeunganishwa na huduma ya umeme na mpaka sasa ni vijiji 10,324 kati ya 12,268 Tanzania Bara.

Alisema pamoja na kuendelea na ukamilishaji wa vijiji hivi sasa, pia wanaendelea kuunganisha umeme katika baadhi ya vitongoji nchini.

"Idadi ya vijiji vilivyobaki ni kidogo, hivyo sasa wakati huu pia tunaendelea na kupunguza idadi ya vitongoji ambavyo havina umeme," alisema.

Kadhalika alisema kuwa katika kikao hicho na timu ya wafadhiri pia wanafanya mazunguzo ili kupata kiasi cha fedha ambacho kitasaidia kusambaza huduma ya umeme katika maeneo ya vitongoji.

"Kusambaza umeme katika vitongoji vyote nchini ni takribani Sh. trilioni 8.8 hivyo kiasi hichi ni kikubwa, hivyo tunahitaji pia wadau wengine kutushika mkono," alisema.

Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja, aliwataka wananchi kuitumia miradi hiyo ya umeme na kuilinda kwa kuwa serikali imekuwa ikitoa kiasi kikubwa cha fedha kuiendesha.



## Waziri abainisha hali ya kesi za mihadarati

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KESI nyingi za tuhuma za watu kukamatwa na uingizaji wa dawa za kulevya zimeishia mahakamani pamoja na ngazi ya upelelezi wa Jeshi la Polisi huku zingine zikifutwa kwa kukosa ushahidi wa kuwatia hatiani watuhumiwa.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Dk. Sada Mkuya, alisema jana wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2021/22 katika Baraza la Wawakilishi, Chukwani nje ya mji wa Zanzibar.

Dk. Mkuya alisema kuanzia Januari hadi Desemba mwaka 2020, kesi 214 zilifikishwa mahakamani na zilizobainika watuhumiwa wana hatia ni 28 na watuhumiwa watano kuachiwa huru. Pia alisema kesi zilizofungwa na Jeshi la Polisi kwa maana ya kufutwa ni 18.

Alisema kesi zilizofikishwa katika Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) ni 13 na kesi zilizoko chini ya upelelezi wa polisi ni 140.

Katika kipindi hicho, alisema wageni saba walikamatwa na tuhuma za kuingiza dawa za kulevya zenye uzito wa kilogramu 22.7 na kesi nne ziko mahakamani, moja imehukumiwa kifungo cha miaka 14 jela na moja imefutwa na zingine kifungo miaka 25 na faini ya Sh. milioni 20.

Dk. Mkuya alisema kwa mujibu wa uchunguzi uliofanywa kujua sababu kubwa ya kesi hizo kuchelewa kukamilika upelelezi wake, ni watendaji wengi wa Jeshi la Polisi kutokuwa na utaalamu wa kutosha wa kuchunguza.

"Mheshimiwa tumefanya utafiti mdogo kutaka kujuwa sababu za kesi nyingi za dawa za kulevya kuchelewa kukamilika uchunguzi. Tumebaini baadhi ya watendaji wa Jeshi la Polisi hawana utaalamu na uwezo wa kutosha wa kufanya uchunguzi katika maeneo ya dawa ya kulevya," alisema.

Hata hivyo, alisema Tume ya Taifa ya Kuratibu na Kudhibiti Dawa za Kulevya iko katika mchakato wa kuteketeza dawa za kulevya zenye jumla ya kilo 124.024.



Mwakilishi wa Jimbo la Chaani, Nadil Abdullatif akiangalia kitabu cha hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ya mwaka 2021/2022, wakati Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman (hayupo pichani), akiwasilisha bajeti hiyo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Sakata vileo latinga Baraza la Wawakilishi

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

MJADALA mzito umeibuka Baraza la Wawakilishi baada ya serikali kutakiwa kuivunja Bodi ya Udhibiti Vileo kutokana na kutoa vibali kwa kampuni 10 vya kuigiza pombe Zanzibar badala ya tatu.

Hatua hiyo, imeelezwa kuwa ni kinyume na Sheria ya Vileo Namba 9 ya mwaka 2020.

Mjadala huo uliibuliwa jana na Mwakilishi wa Ziwani, Suleiman Makame Ali, Mwakilishi wa Chaani, Nadir Abdulratifu na wa Chake-chake, Shaib Hassan Kaduara, wakati wakichangia makadirio na matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa mwaka wa fedha wa 2021/22.

Suleiman alisema Bodi ya Vileo Zanzibar imevunja kifungu cha 33(1) cha Sheria ya Vileo baada ya kutoa vibali kwa kampuni 10 badala ya tatu kinyume cha sheria iliyopitishwa na Baraza la Wawakilishi na kuanza kutumika baada ya kutiwa saini na Rais wa Zanzibar Mei 11, mwaka jana.

"Mheshimiwa Spika, Bodi ya Vileo imekwenda kinyume cha sheria hii. Sasa kama leo (jana) bodi hiyo inastahili kufutwa na viongozi kujiuzulu kabisa akiwamo mwenyekiti na wajumbe wake. Hawafahi kwa sababu hakuna kifungu kilichomruhusu kuongeza kampuni," alisema Suleiman.

Alisema viongozi au watendaji wakuu wa serikali wanatakiwa kusimamia sheria katika misingi ya utawala bora na si kuvunja sheria iliyopitishwa.

"Mheshimiwa Spika sisi tunapotunga sheria katika nchi yetu tunaomba sana sheria hizi ziheshimike na hakuna mtu yeyote ambaye anaweza kutokea kwenda kinyume cha sheria au kujifanya yeye anaweza kufanya uamuzi zaidi ya Baraza la Wawakilishi," Nadir.

Alisema lengo la serikali kutungwa sheria ya udhibiti wa Vileo Zanzibar lilikuwa kupunguza matumizi ya pombe pamoja na kuweka utaratibu mzuri wa kisheria wa uigizaji badala ya vileo kuigizwa holela pamoja na kudhibiti uanzishwaji wa baa karibu na maeneo ya huduma za jamii. Nadir alisema kifungu cha 28(k) kimeweka sharti la baa kupewa leseni kwamba lazima iwe umbali wa mita 1,000 kutoka maeneo ya huduma za jamii kama shule, hospitali, nyumba za ibada na makazi, lakini bodi imeshindwa kusimamia masharti ya sheria hiyo.

"Mheshimiwa Spika, sijui Mwenyekiti wa Bodi mamlaka haya amepewa na nani maana yake angefanya Rais tungeheshimu kwa sababu bosi wetu anaweza. Lakini anafanya mtu wa chini kulipinga Baraza la Wawakilishi wakati Makamu wa Pili wa Rais yumo ndani ya baraza," alisema Nadir.

Alisema vibali vyote vilivyotolewa kinyume cha sheria vinapaswa kufutwa kulinda sheria na waziri mwenye dhamana kuchukua hatua dhidi ya watendaji walioshiriki kuvunja sheria. Kaduara kwa upande wake alisema kitendo kilichofanywa na Bodi ya Vileo Zanzibar kinakwenda kinyume cha misingi ya utawala bora katika mgawanyo wa madaraka kati ya Baraza la Wawakilishi, serikali na mahakama.

Alisema watendaji wakuu wa serikali wanatakiwa kusimamia utekelezaji wa sheria zinazotungwa na Baraza la Wawakilishi pamoja na kulinda mila na utamaduni ndiyo maana serikali imetunga sheria ya udhibiti wa vileo Zanzibar.

# SMZ yasitisha utoaji leseni za meli

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) imesema Mamlaka ya Usafiri wa Baharini Zanzibar (ZMA) imesitisha kufanya usajili wa kutoa leseni kwa meli za nje baada ya kubainika meli zilizopewa usajili kukiuka sheria na kujishughulisha na kusafirisha dawa za kulevya na silaha.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, anayeshughulikia Uratibu na Baraza la Wawakilishi, Dk. Khalid Salum Mohamed, wakati akitoa ufafanuzi kuhusu hoja iliyotolewa na Mwakilishi wa Shauri Moyo, Hamza Hassan Juma.

Mwakilishi katika swali lake, alitaka kujua lini suala la Zanzibar kuendelea na shughuli za usajili wa meli za kimataifa itaruhusiwa.

Waziri huyo alisema meli zilizokuwa zikipewa leseni kwa ajili ya usajili zilikuwa zikipeperusha bendera ya Jamhuri ya Muungano na ndipo baadhi ya nchi na mashirika ya kimataifa zilipowasilisha malalamiko kuhusu kadhia hiyo kwa serikali ya Muungano.

Alisema baada ya uchunguzi ilibainika kuwapo kwa kasoro hizo ndipo serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilipochukua uamuzi kwa upande wa Zanzibar kupitia ZMA kusitisha shughuli za kutoa leseni kwa ajili ya kupisha uchunguzi.

"Mheshimiwa Spika ni kweli ZMA imesitisha shughuli na kazi za kutoa leseni na usajili wa meli za nje baada ya kujitokeza kasoro mbalimbali ikiwamo meli tulizozipa leseni kusafirisha dawa za kulevya na zingine kubeba silaha," alisema.

Alisema suala hilo liko katika mikono ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa ajili ya uchunguzi zaidi na kufanyiwa kazi na kwamba ni matumaini ya Zanzibar suala hilo litamalizika na kuruhusiwa kuendelea kufanya shughuli za usajili.

Waziri alisema mazungumzo yanaendelea kwa pande mbili za Muungano kuhusu suala hilo na ni matumaini makubwa kadhia hiyo itapatiwa ufumbuzi.

"Mheshimiwa Spika napenda kuwajulisha wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba suala la Zanzibar kuzuiwa kutoa leseni kwa meli za nje kufanya usajili lipo katika ngazi ya mazungumzo," alisema.

ZMA miongoni mwa majukumu yake, ni kutoa leseni ya vibali kwa meli za nje kutoa huduma za usafiri na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilisitisha kazi hizo mapema mwaka 2016.



**LULU DIVA ARINGIA URITHI WA MAMA** Uk.12

Nipashe MWANGA WA JAMII
BT
JUMAMOSI MEI 8, 20



**IMETOSHA!**

# Nani kakua kisanaa kuimba uchafu?

MJADALA mkali unazidi kushika kasi katika tasnia ya sanaa, baada ya serikali kuagiza kazi zote sasa zitahakikiwa kabla ya kuruhusiwa kutoka kwa wananchi.

Agizo hilo limeleta sitofahamu kwa wasanii wa muziki na uigizaji, huku wengi wao wakipinga wakidai hatua hiyo itachelewesha au kukua sanaa hapa nchini.

Hata hivyo serikali kupitia Baraza la Sanaa Tanzania (BASATA) imesisitiza kanuni hiyo itarudisha maadili ya kisanii kutokana na baadhi kutengeneza kazi ambazo maudhui yake hayawezi kuwekwa wazi kwa jamii kutokana na kujaa maneno yenye ukakasi.

Wanaopinga wanaeleza kutokana na ufinyu wa wafanyakazi, BASATA haitaweza kuhakiki kazi zote wanazotoa wasanii na hapo ndipo ucheleweshaji utakapotokea na kusababisha wao kupata hasara.

Katika kile ambacho kinaonekana kugomea kanuni hiyo, rapa Nay wa Mitego, alikiuka kwa kusambaza wimbo wake 'Mama' katika mitandao ya kijamii huku akisisitiza hawezi kuupeleka.

**NANI WA KULAUMIWA?**

Hata hivyo, lawama zote zinawaangukia wasanii wenyewe kwani siku za hivi karibuni wamekuwa wakitumia lugha za matusi na zenye kukera katika nyimbo zao au filamu.

Imekuwa jambo la kawaida kwa mwanaumuziki katika nyimbo zao kuimba viungo vya binadamu au matendo ya faragha kwa uwazi, jambo ambalo limesababisha kusikilizwa na watu wa aina moja.

Wameshindwa kujifunza na wasanii wa zamani ambao nyimbo zao bado zinaendelea kuishi kutokana na kutumia lugha ya mafumbo na tafsida ili kukidhi watu wa aina zote.

**USHAMBA**

Mwanamuziki mkongwe Khalid Mohamed, maarufu kama TID, anasema kuna ushamba katika sanaa kiasi ambacho baadhi ya wasanii wanaona kuimba uchafu kama kukua kimuziki.

"Kwenye muziki kimaadili haitakiwi kupromote uchafu, kuhakiki naona hapo wameanza kufanya kazi labda hawajatoa ufafanuzi wa jinsi gani wataweza kumudu kwa ukubwa." Amesema.

Hata hivyo, wasanii wakubwa kama Diamond Platnumz na Ali Kiba, ambao watu wengi walitarajia kusema chochote, bado wamekaa kimya mpaka sasa.

BASI SAWA

## Domokaya azindua mbili kiaina

MWANAMUZIKI mkongwe nchini, Domokaya, ametambulisha nyimbo zake mbili "My chick" na "I care", huku akijigamba amepewa Baraka na serikali.

Akitambulisha nyimbo hizo katika kipindi cha Planet Bongo cha East Africa Radio, msanii huyo alionyesha barua kutoka Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) ya kumruhusu kuzitoa kwa umma kusikiliza.

Domokaya ni moja kati ya wasanii wachache waliofuata taratibu hizi mpya za BASATA ambazo zimeonekana kupingwa na wasanii wengi tangu zilipotangazwa.



## Superman mweusi kuja kama hivi..



DUNIA inabadilika kwa kasi, sasa ubaguzi wa rangi katika tasnia ya sanaa unaanza kuyeyuka taratibu kama theluji.

Wiki hii imetolewa taarifa ya kutia moyo baada ya watengenezaji wa filamu maarufu duniani 'Superman' kueleza nia yao ya kumhusisha mtu mweusi.

Warner Bros na DC wamesema filamu ijayo ya Superman atakuwa na mwonekano wa mtu mweusi na hivyo kuondoa dhana iliyojengeka kwamba wahusika wa filamu hiyo ni wazungu pekee.

Waongozaji hao wamejitolea kuajiri mkurugenzi mweusi ili kuratibu shughuli zote za Superman ijayo akishirikiana na waigizaji weusi.




## Lulu Diva aringia urithi wa mama

MSANII wa muziki wa Bongo Fleva, Lulu Diva, amemkumbuka mama yake kwa kuandika maneno ambayo hupenda kumweleza wakati wanapokuwa pamoja.

Lulu Diva amesema mama yake huwa anapenda kumwambia asikate tamaa, apambane na aongezee bidii kwenye kazi pia kauli nyingine anayopenda kumuhusia ni ile asifananishe kifo na usingizi kwa sababu ni vitu viwili tofauti.

"Mama yangu anatoa sapoti kubwa sana japo hawezi kufanya vitu vingi kwa sababu sasa hivi ni mgonjwa, anapenda kuniambia nisikate tamaa, nifanye kazi kwa bidii, na nipambane halafu ana neno lake moja ambalo anapenda kuniambia kwamba nisifananishe kifo na usingizi" amesema





## Filbertha awapa neno wadau wa urembo

MKUFUNZI na mrembo Filbertha Juma, amesema kuna tabia inayofanywa na baadhi ya waandaaji kutokabidhi zawadi za ushindi wa warembo na kusababisha tasnia hiyo kuonekana ya kitapeli.

Akizungumza mara baada ya kuteuliwa na kamati ya Miss Dodoma kuwa mkufunzi wa kuwanoa walimbwende hao, amesema kwa upande wake hajawahi kukutana na hali hiyo, lakini wapo baadhi wanalalamika.

"Kwa upande wangu sijawahi kukumbana na hali hiyo ila napenda kusisitiza wadau kukabidhi zawadi za washindi kwa wakati kuliko kuchelewesha jambo linalosababisha kuvunjiana heshima, tukio kama hilo linaichafua tasnia yetu siku hadi siku, hii ni ajira na inaajiri watu wengi na imeshatoa viongozi akiwamo Jokate Mwegelo, Chuchu Hansy na wengine," alisema.

## Madudu filamu za Kibongo

**Na Adam Fungamwango**

KUMEKUWA na ongezeko kubwa la Wabongo kuangalia zaidi tamthilia za Kihindi, Kikorea, Kifilipino na hata Kichina. Kwenye filamu wanaangaliza zaidi za Kizungu, Kichina, Kinaigeria na Kihindi.

Wapo wanaoangalia tamthilia za Kitanzania ambazo nazo zinaonekana angalau zenyewe zinafanya vizuri, lakini kumeonekana kushuka kabisa biashara ya filamu.

Ndiyo maana mastaa wengi wa Bongo Movie kwa sasa wanacheza tamthilia. Zipo sababu nyingi za kushuka kwa mauzo ya filamu, na Watanzania kutopenda kuziangalia tena.

Ni kwa sababu tayari wameshaonja tamthilia kutoka nje ya nchi, hasa zilipoanza kutafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili. Wabongo wameanza kuona aina tofauti ya uigizaji, wenye uhalisia wa hali ya juu, pamoja na uandishi wa hadithi wenye upeo wa hali ya juu. Visa na mikasa wanavyoviona ni vile ambavyo vipo kwenye jamii, japo imetofautiana mazingira kutokana na nchi husika.

Huku kwetu filamu nyingi zinafanana sana. Ni lazima mtu akitoka kijijini masikini lazima awe tajiri, au aoe au aolewe na mtu tajiri.

Upungufu uliopo kwenye filamu za Kibongo unasababisha Watanzania wenyewe kuwa na dhihaka mbalimbali ambazo wanazitoa kuonyesha kutoridhishwa na jinsi wanavyoigiza.

**KILA MLINZI LAZIMA AWE 'CHALE'**

Hii imekuwa kama utamaduni kwenye filamu zetu. Na sijui nani ameanzisha. Na waongozaji wa filamu wote wamekariri. Eti mlinzi wa getini ni lazima awe kama vile zimemruka hivi.

Ukiangalia filamu nyingi, utakuta walinzi wa getini wanakwenda wasanii wa vichekesho, au watu ambao ni lazima wacheze kama 'chale', huku nguo zao zikiwa kuukuu. Hii inaboa na kuzifanya sinema zetu kuzoeleka na kutabirika.

**ANARUDI ULAYA NA NGUO ILE ILE**

Hapa nadhani tatizo ni bajeti. Lakini inapoteza sana uhalisia. Mhusika anakwenda Ulaya. Halafu anaonyeshwa anarejea anashuka Uwanja wa Ndege akiwa na nguo hiyo hiyo aliyokwenda nayo miaka mitano iliyopita. Tena siyo nguo tu, ila mwonekano ni ule ule. Kiuhalisia haikupaswa kuchukua picha mhusika anasafiri na kurejea siku hiyo hiyo. Ilibidi wakae hata wiki. Abadilishe nguo na mwonekano.

**ANAKUMBUKA ZAMANI, PICHA RAIS MPYA**

Upungufu mwingine ni kwamba inawezekana mhusika akawa anakumbuka zamani alivyokuwa kijana au mtoto. Lakini unaweza kukuta picha za ukutani nyumbani kwao au ofisini ni za rais wa sasa.

Uhalisia hapo unapotea kwani mtu anajiuliza, anakumbuka vipi zamani wakati picha za ukutani zinaonyesha Rais anayoongoza hivi sasa. Huu ni uvivu wa kufiriki kwa waongozaji. Ilibidi watafute picha wa Rais ambaye wao walitaka kuonyesha mwaka huo. Au kama vipi ziondolewe wakati uchukuaji wa picha.

**GEREZA, KITUO CHA POLISI VICHEKESHO**

Wakati wenzetu ukikuta mhusika yupo gerezaji au kituo cha polisi kuna uhalisia mtupu, tofauti na hapa kwetu.

Hii siwalaumu sana kutokana na jinsi tu sanaa yenyewe inavyochukuliwa Bongo. Kwa wenzetu wanaweza kuruhusiwa kuigizia kwenye kituo cha polisi mradi tu masharti yafuatwe. Pia kuna watu binafsi wanajenga vitu kama hivyo kwa ajili ya kukodisha kwa kampuni za kuigizaji.

**JAMBAZI LAZIMA AVAE KOTI REFU**

Kwa hali ya kawaida kabisa, mtu yoyote muovu huficha uhalisia wake wa moyoni. Kwenye filamu za Kibongo mtu yoyote muovu hasa jambazi ni lazima avae koti refu jeusi na mawani meusi. lengo siyo baya, kuweka uhalisia. Lakini si kila filamu mhusika anatakiwa ajulikane kuwa mtu mbaya hata kwa mwonekano.



## Ndiyo Ukome; la mchana, wenzako la usiku

**Na Adam Fungamwango**

KUNA watu wana tabia ya kuwafanyia wenzao mabaya wakidhani kuwa wao hawawezi kupata matatizo. Wanadhani kuwa mabaya wameumbiwa wenzao tu.

Siku wao yakiwapata, dunia nzima itajua kuwa wana matatizo. Hawajui kuwa Mungu ni wa wote.

Leo tunaiangalia filamu iitwayo 'Ndiyo Ukome.' Ni filamu yenye mafunzo kwa watu ambao wanafanya mambo bila kutafakari mbele.

Msichana Nancy anakutana na mpenzi wake Steve, akimtaarifu kuwa ni mjamzito. Steve anaruka futi mia kuwa siyo ya kwanza. Cha zaidi anamwambia kuwa hampendi na hajawahi kumpenda. Tena akamwambia kuwa mpenzi wake huyo kuwa mimba ile si ya kwake kwa sababu amepata taarifa kuwa anatembea na wanaume wengi sana.

Nancy akaangua kilio. Alifikiria siku ya kwanza kukutana alivyomwahidi kuwa anampenda, atampenda, atamlinda, atamtunza na kumsikiliza pia. Leo hii kumbe yote ni uongo.

Anakwenda kumwambia baba yake. Baba Nancy na binti wake wanakutana na Steve. Kijana huyo anawatolea maneno ya kashfa binti na baba yake.

Baba Nancy hakukubali. Akamchukua binti yake hadi nyumbani kwa kina Steve. Huko anamkuta baba yake. Baba naye kama mwanaye tu. Akamtolea mzee mwenzake maneno ya kashfa.

Mzee akarudi nyumbani na binti yake. Hakusema kitu. Siku si nyingi Steve alianza kutapika na kula mkaa. Watu wakaanza kushangaa kwa nini mwanamume anakuwa kwenye hali hiyo. Akaenda hospitali kupima vipimo vikaonyesha kuwa ni mjamzito. Hali hiyo siyo tu ilimfanya kuumwa, lakini pia ilimtia aibu kijijini hapo.

Ndipo alipojua kabisa kuwa baba Nancy amefanya kazi yake. Baba Steve na kijana wake waliogopa kwenda kumwomba radhi kutokana na yale ambayo waliyasema, na kumkashifu yeye na binti yake.

Hali ilikuwa mbaya, Steva akaamua mwenyewe kwenda kwa mpenzi wake Nancy kuomba msamaha, lakini anatimuliwa.

Baba Steve sasa ilibidi aunde jopo kwa kumshirikisha hata mjumbe wa nyumba kumi na watu wengine wazee kwenda kumuomba na kumpigia magoti baba Nancy ili ategue tego la kumpa ujauzito kijana aliyempa mimba binti yake.



# Tristan hawezi kujiokoa kwa hili



MCHEZAJI wa mpira wa kikapu Tristan Thompson, anapanga kumchukulia hatua za kisheria mrembo Sydney Chase, kutokana na madai yake kuwa walikuwa wanatoka kimapenzi wakati staa huyo yupo katika uhusiano na Khloe Kardashian.

Mrembo huyo wiki iliyopita alidai Tristan alimdanganya kuwa hakuwa na mke wakati wakiwa katika uhusiano wa kimapenzi, kumbe alikuwa na mke na mama mtoto ambaye ni Khloe.

"Ndio, tunakwenda kufungua mashtaka na kufuta yote, tunahitaji mambo yawe ya ukweli na sio kuharibu uhusiano wa watu wengine," amesema Adam John, ambaye ni mshauri wa kisheria wa Tristan.



## Hongera Skales kuvuta jiko

MWANAMUZIKI mkali wa Nigeria, Raoul John Njeng-Njeng, anayejulikana kama Skales, amefunga ndoa na mpenzi wake ambaye ni mwanamitindo.

Skales na amefunga ndoa ya kimila na mchumba wake na kuhudhuriwa na mastaa mbalimbali akiwamo Harmonize kutoka Tanzania.

Mwanamuziki huyo aliposti video fupi katika mtandao wa Instagram, ikionyesha jinsi sherehe hiyo ilivyofana.

## Kizz Daniel watunze mapacha wako

MWANAMUZIKI kutoka Nigeria, Oluwatobiloba Daniel Anidugbe, maarufu kama Kizz Daniel, amekuwa na furaha baada ya kupata watoto mapacha.

Nyota huyo wa muziki ametoa habari hiyo kupitia mtandao wa Instagram, akisema yeye na mpenzi wake wamebarikiwa kupata watoto wawili wakati akisherehekea siku yake ya kuzaliwa.

"Si jambo baya kufurahia siku yangu ya kuzaliwa huku nikiwakaribisha na kuwatambulisha watoto wangu Jelina na Jalil," ameandika.





## Burna Boy huu ni mwaka wako

MSHINDI Wa tuzo ya Grammy, Burna Boy, mwaka huu umekuwa wake baada ya wimbo wake "Ye" wa mwaka 2018, kufikia mauzo ya dhahabu.

Kulingana na Chama cha Kurekodi Muziki cha Marekani, (RIAA) umepata ngazi hiyo baada ya albam wenye wimbo huo 'Outside' kuuzwa nakala 500,000

Mwaka 2019 Burna boy alishinda tuzo ya wimbo bora wa mwaka na chaguo la msikilizaji kwenye Soundcity MVP Awards Festival na The Headies kupitia wimbo wa "Ye".

## Baba Ijeshi kuburuzwa mahakamani

SERIKALI ya jimbo la Lagos,imepanga kumfungulia mashtaka ya ubakaji mwigizaji Baba Ijesha, aliyofanya miaka saba iliyopita.

Ofisi ya mwendesha mashtaka (DPP), imesema msanii huyo atafunguliwa kesi kulingana na kifungu cha sheria namba tano ya kesi ya jinai ya jimbo hilo.

Katika maelezo yake Kamishna wa mahakama, Moyosore Onigbanjo on, amesema Baba Ijesha, atawajibika kujibu mashtaka hayo kutokana na jaribio la kumbaka binti wa mchekeshaji.



MAKALA

# Udhibiti ulivyoboresha huduma za majisafi na usafi wa mazingira

## •Ni mkakati mahususi wa EWURA katika kuondoa kero kisekta

Na Mwandishi Wetu

MAJI ni uhai. Huu ni msemo ambao umekuwa maarufu katika jamii kutokana na umuhimu wa huduma hiyo katika maisha ya wanadamu.

Hiyo inatokana na ukweli kwamba shughuli nyingi za kibinadamu kwa kiasi kikubwa zinategemea maji. Iwe katika mazingira ya kifamilia au uzalishaji viwandani na huduma katika elimu na afya. Bila maji ni vigumu shughuli hizi kuendeshwa.

Mfanyabiashara maarufu nchini, Ali Mufuruki (sasa marehemu) katika moja ya mada zake aliwahi kusema: "Kama kutakuwa na vita kuu vya tatu vya dunia, basi vitatokana na kugombania maji." Yote hiyo inatokana na umuhimu wa bidhaa au huduma hiyo kwa maisha ya wanadamu.

Nchini Tanzania, kama ilivyo katika mataifa mengine, maji ni jambo la muhimu ili kufanikisha mambo mengi kuanzia ngazi ya familia hadi taifa. Ndiyo maana sekta hiyo inapewa kipaumbele kwa maendeleo ya taifa na kutokana na hali hiyo, fedha nyingi zimetengwa kwa ajili ya miradi ya maji.

Ili kuhakikisha kunakuwa na matumizi yasiyoathiri maisha ya watu na kudhibiti uharibifu katika huduma hiyo adhimu, serikali imeanzisha vyombo vya usimamizi husan mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira pamoja na miradi ya kitaifa ya maji.

Licha ya mamlaka hizo kuwa wasimamizi wa huduma za maji, pia serikali mwanzoni mwa miaka ya 2000 ilianzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA). Mbali na maji, EWURA pia inadhibiti huduma za umeme, mafuta na gesi.

Kuwapo kwa mamlaka hiyo kumewezesha udhibiti wa huduma za maji ikiwamo upangaji wa bei usioumiza wateja. Udhibiti huo pia ni shirikisha kwa maana ya wadau kuhusika katika maoni ya mabadiliko ya bei na pia kutoa malalamiko pale huduma zinapokuwa si za kuridhisha.

**HALI KABLA**

Kabla ya kuanzishwa kwa mamlaka hiyo, lilikuwa na upandaji holela wa bei za maji, mafuta (petroli, dizeli na mafuta ya taa), majisafi na usafi wa mazingira.

Hatua hiyo iliwakandamiza watumiaji wa bidhaa kwa upande mmoja na kuwanufaisha watumia huduma pamoja na wafanyabiashara upande mwingine. Wafanyabiashara walijiona ni miunguwatu kwa kupandisha bei holela.

Kuanzishwa kwa EWURA kumesaidia kuwapo kwa udhibiti wa hali ya juu wa huduma hizo, zikiwamo za majisafi na majitaka katika maeneo mbalimbali husussan kwenye maeneo ya mijini.



Mtambo wa maji wa Ruvu Juu.

Uwapo wa mamlaka hiyo umesaidia upandishaji au mabadiliko ya bei ya huduma hizo kupitia kwa wadau wakiwamo watumiaji kabla ya kuanza kutumika.

Kuhusu udhibiti wa huduma hizo, taarifa ya EWURA inabainisha kwamba hadi Juni 30, 2020, EWURA inadhibiti mamlaka 25 za mikoa za maji na usafi wa mazingira, mamlaka 16 za wilaya za majisafi na usafi wa mazingira na miradi minane ya kitaifa.

**MATOKEO YA UDHIBITI**

Katika sekta ya maji, EWURA imekuwa na mafanikio katika kuboresha utendaji wa mamlaka nyingi kifedha na kiutawala. Kabla ya hapo, mamlaka nyingi zilikuwa hazina uwezo kiutendaji kiasi cha kushindwa kutoa huduma zinazostahili na kwa viwango.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka hiyo, Mhandisi Godfrey Chibulunje, anasema kabla ya usimamizi na udhibiti thabiti, utendaji katika mamlaka nyingi ulikuwa hafifu, hivyo kusababisha utoaji huduma kuwa duni.

"Mamlaka nyingi zilishindwa kujiendesha kwa sababu ya ukosefu wa fedha na utaalamu. Lakini kutokana na jitihada zilizofanyika, ikiwamo kuzijengea uwezo, hali sasa imebadilika kwa kiasi kikubwa na huduma za majisafi na usafi wa mazingira zimeimarika kwa kiasi kikubwa," anasema Chibulunje.

Katika ripoti ya utendaji ya mamlaka za maji ya mwaka 2015/16, kwa mfano, utendaji ulikuwa asilimia 43.1. mbali na utendaji na uwezo wa kifedha, hatua hiyo ilisababishwa pia na ukusanyaji mdogo wa maduhuli kutokana na utumiaji wa huduma za maji.

Miongoni mwa mambo yaliyofanyika kuhakikisha viwango vya utoaji huduma vinapanda ni pamoja na kutoa mafunzo kwa watendaji wa mamlaka baada ya kutokuridhishwa na utendaji kutokana na ripoti hiyo ya mwaka 2015/16.

Sambamba na hiyo, anasema EWURA imetoa mafunzo na kuwezesha mamlaka za maji kuandaa mipango ya kibiashara inayolenga kuboresha huduma za maji. Awali mamlaka hizo zilikuwa zikiendeshwa bila utaratibu na watendaji kufanya kazi kwa mazoea huku kukiwa hakuna dira na malengo chanya ya utoaji huduma.

"Mamlaka zimeongeza uwezo wa kiufundi, kiutawala na kifedha. Mamlaka 84 kati ya 130 zimeandaa mipango yao kibiashara na mamlaka 39 zimekuwa na bei za maji zinazozingatia mipango ya biashara ya miaka mitatu.

"EWURA pia imezijengea Mamlaka za maji ushindani wa kiutendaji. Kila mwaka, mamlaka hizi hushindanishwa kwa vigezo mbalimbali. Hii imetoa chachu kwa mamlaka nyingi kutoa huduma bora na kwa ufanisi zaidi," anasema.

Hatua hiyo imezaa matunda kutokana na yaliyojiri katika ripoti ya utendaji ya mamlaka ya mwaka 2018/19 iliyojumuisha mamlaka 36 za mikoa za majisafi na usafiri wa mazingira, mamlaka za wilaya 83 na miradi ya kitaifa ya maji.

Ripoti hiyo, pamoja na mambo mengine, inabainisha kwamba utoaji wa huduma umeimarika katika kiwango cha maji yanayozalishwa na idadi ya watu wanaopata maji, ubora wa maji na uondoaji wa majitaka.

Katika kuhakikisha huduma zinatolewa kwa kiwango kinachotakiwa, mamlaka pia imekuwa ikitoa ushauri kwa serikali wa hatua zinazohitaji kuchukuliwa kuboresha mamlaka za maji mfano. Pia kuunganisha mamlaka ndogo ili kuleta tija katika kutoa huduma za maji na kupunguza bei za maji kwa wananchi

Ili kuwezesha pia kunakuwa na utendaji bora, Chibulunje anasema, EWURA huzitaka mamlaka za maji kuwa mkataba wa huduma kwa wateja na hilo limefanikisha wananchi kuwa na uwezo wa kudai haki zao kulingana na mikataba hiyo.

**CHANDA CHEMA**

Wahenga wanasema chanda chema huvikwa pete. Hivyo ndivyo ambavyo EWURA imekuwa ikifanya kwa kutoa tuzo kwa mamlaka ambazo zinafanya vizuri katika utoaji wa huduma za maji.

Kutokana na azma hiyo ya kuzawadia mamlaka vinara katika utoaji wa huduma, Mwenyekiti wa Bodi ya EWURA, Ahmad Kilima, anasema tuzo hizo zinatolewa kutokana na ushindanishaji katika viashiria vya kiutendaji husussan katika utoaji huduma na mikataba ya huduma kwa wateja.

Mwaka jana kwa mfano, kutokana na vigezo vilivyowekwa katika upatikanaji wa washindi, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira ya Moshi ilishika nafasi ya kwanza kitaifa kwa mamlaka za mikoa, ikifuatiwa na Iringa na Mwanza.

Kwa upande wa miradi ya maji ya kitaifa, KASHWASA (Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kahama na Shinyanga) ziliibuka kidedea ikifuatiwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira ya Masasi-Nachingwea (MANAWASA) na ile ya Chalinze. Kwa mamlaka za miji midogo na wilaya, zilizopata tuzo kwa kufanya vizuri ni Makambako, Mikumi na Biharamulo.

"Moshi, Makambako na KASHWASA zilipata tuzo kutokana na kufikia malengo ya kiutendaji katika utoaji wa huduma za majisafi na usafi wa mazingira. Shinyanga, Maganzo na KASHWASA zimekuwa vinara katika udhibiti wa upotevu wa maji," inabainisha taarifa ya EWURA kuhusu tuzo hizo.

Aidha mamlaka za Moshi, Iringa, Dodoma, Makambako, Usa- River na Dakawa, zilipata tuzo kutokana na uwasilishaji wa tozo za udhibiti.

Pamoja na kuboreshwa kwa utoaji huduma za majisafi na usafi wa mazingira katika mamlaka, bado kuna kero au vikwazo ambavyo vinapaswa kupatiwa ufumbuzi ili kutoa huduma kwa viwango vya juu zaidi. Miongoni mwa kasoro hizo ni kuendelea kuvuja kwa maji kutokana na uchakavu wa mabomba, wateja kujiunganishia maji na kuchezea mita.

## KATA YA MFANO MAGU...

# Wazazi walivyokomboa watoto kila siku safari Km. 38 kufuata masomo

**Na Anthony Gervas, MAGU**

## ●Hoi; kuvuka mto, mvua, 'mafataki'... ●Mtaji michango, shule ya pili yaja



Shule ya Sekondari ya Kata Buhumbi, wilayani Magu.

TANZANIA, kama zilivyo nchi nyingi za dunia ya tatu, inakabiliwa na shida nyingi kukabili matatizo ya kijamii na kimaendeleo.

Tangu kutoweka haki ya elimu bure kwa miongo kadhaa tangu uchumi huria ulipochukua hatamu mwaka 1985, Rais Dk. John Magufuli alipoanza kuongoza nchi mwaka 2015, alirejesha elimu bure kuanzia elimu msingi hadi sekondari kidato cha nne, ikiendelea hadi sasa katika awamu ya sita ya uongozi.

Lengo la serikali ni watoto wa kitanzania wanufaike na fursa ya shule zao kutokana na uhalisia familia nyingi ni maskini, zisizokuwa na uwezo kuwasomesha, hivyo ikaleta mfumo wa elimu bila malipo.

Ni kati ya mipango ya kiserikali inayonuia kutokomeza adui ujinga, sambamba na miradi mingine ya maendeleo kama vile kuwapo wingo wa zahanati, vituo vya afya na hospitali, huku wananchi wakiunga mkono jitihada hizo.

**WAZAZI WAAMUA**

Wazazi wa Kata ya Buhumbi wilayani Magu, mkoa wa Mwanza, wameamua kubeba jukumu hilo kwa kujipanga kuhakikisha wanaiunga mkono serikali katika utekelezaji miradi yake maendeleo na kutatua changamoto zinazowakabili wanafunzi shuleni, hususani sekondari za kata.

Diwani wa Kata ya Buhumbi, Petro Matonange, anaelezea ujenzi wa shule ya sekondari iliyofunguliwa kwenye kata yao, imewaondolea kero wanafunzi kutembea umbali kilomita 19 kwenye kata jirani ya Sukuma.

"Wazazi tumechangia ujenzi huo zaidi ya Sh. milioni 30 na serikali imetusaidia Sh. milioni 20," anabainisha Diwani Matonange.

Anasema umbali kwenda shuleni na kurudi nyumbani, waliotembea wanafunzi hao ni sawa na kilomita 38, huku kukiwapo mazingira yasiyo rafiki ya usafiri, wanavuka mto na kunyeshewa na mvua wakati wa masika.

Kwa mujibu wa diwani huyo, uchungu wa elimu kwa watoto wao katika kata hiyo, kuna jumla ya kaya 786 zimechangia kila moja Sh. 41,000 na diwani amechangia fedha na saruji mifuko 30; Mbunge wa Magu, Bonventra Kiswaga alichanga saruji mifuko 100.

Diwani anasema, ujenzi wa shule hiyo ulianza mwaka 2018, baada ya Kata ya Sukuma kugawanywa na kuzaliwa kata mpya ya Buhumbi, ukijumuisha vyumba vinne vya madarasa, ambavyo havijakamilika, kukiwapo matarajio vilivyosalia kukamilishwa mwaka huu.

Anasimulia machungu ya safari za wanafunzi kwenda kata jirani, walitembea umbali wa kilomita 38, kwenda shuleni na kurudi nyumbani, huku mazingira ya usafiri yakiwa siyo rafiki, kuvuka mto na mvua kunyeshewa wakati wa masika ilikuwa ni kawaida kwao.

Hata hivyo, kuna kilio cha madereva wa bodaboda na waendesha daladala za baiskeli, wanatajwa kutumia fursa hizo kuwarubuni kimapenzi wanafunzi mabinti, hata kupatikana mikasa ya mimba na masomo yanafikia tamati.

Diwani huyo anaeleza msimamo wake kwamba, ananuia kusimamia ukamilishaji ujenzi wa shule hiyo, akiomba kampuni na mamlaka za kiserikali, pia binafsi kusaidia ujenzi huo.

Mbali na ile inayojengwa, mwakani wanakusudia kuongeza shule mpya ya sekondari katika kijiji cha Misungwi, ili kuwapunguzia adha wanafunzi kutembea umbali mrefu, wakati huohuo shule iliyopo ya Buhumbi, kuwa na kidato cha tano na sita.

Matonange anasema, kuwapo shule mbili za sekondari katika kata hiyo, kutasaidia wanafunzi shuleni kusoma kwa bidii, kuepuka mimba, huku wakielemika kwa ufanisi zaidi.

**MWENYEKITI KIJIJI**

Mwenyekiti wa Kijiji cha Buhumbi kulichojengwa shule, Bernado Patrice, anayataja kuwa mambo yaliyogusa zaidi nafsi yake ni wanafunzi kukata tamaa kuendelea na masomo, kutokana na umbali uliokuwapo wa shule.

Akitumia msamiati kwamba, ni jambo lililomnyima usingizi, anasema yuko katika vita kuhakikisha uchangiaji ujenzi wa shule yao, ili kufuta kabisa shida ya uhaba wa darasa waliokuwa nayo.

Bernado, pia anataja hitaji lingine la maji shuleni kukidhi haja ya wanafunzi na walimu kwa hitaji la matundu 28 kwa jinsia zote mbili, inayolenga zaidi ya wanafunzi 120 watakaoendelea kusoma.

**OFISA ELIMU KATA**

Juma Issa, Mratibu wa Elimu Kata, anaiambia Nipashe kwamba, mbali na mafanikio hayo ya madarasa manne, azma inayofuata: "Mimi nasisitiza tu, ujenzi wa maabara, jengo la utawala na nyumba ya mkuu wa shule."

Ili kufaniksha hilo anabainisha kuwa wazazi wamekubaliana kila kaya kuchangia Sh.15,000 katika ujenzi huo kuanzia msingi hadi kufikia maboma, ikiwa mchango huo utafanyika kwa kaya 786. Pia, serikali itawasaidia kukamilisha uezekaji na upauaji.

Anasema kwamba uhaba wa madawati wazazi wamejitolea kuchanga Sh. 60,000 kila kaya kutengeneza kiti na meza, pia kushirikisha kaya, wadau wa elimu na watumishi wazawa, ambao walishatoa jumla ya shilingi milioni moja na Halmashauri ya Wilaya ya Magu, itasaidia jumla ya madawati 100.

**DED MAGU**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Magu, Lutengano Mwalwiba, anawaasa wanafunzi shuleni, akisema: "Kataeni kurubuniwa na wanaume 'mafataki' waliozoea kuvizia watoto wa shule na kuwapa mimba wakisababisha kuwakatisha ndoto zenu kielimu."

Pia anasema halmashauri yake iko tayari kuendelea kuunga mkono juhudi za wananchi wa Kata ya Buhumbi katika ujenzi wa shule zote zitakazokusudiwa, ili iwe kata ya mfano katika shule zilizopo wilayani humo.

Anawasifia waasisi ambao ni wazazi na wadau wa elimu, kujitoa kufanikisha ujenzi huo, ili kuunga mkono jitihada za Rais Samia Hassan katika sekta ya elimu nchini.

**MWANAFUNZI ANENA**

Zawadi Kabushi, ni mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Buhumbi, anayesimulia magumu, milima na mabonde ya safari ya kilomita 38 za kwenda na kurudi shule kila siku.

"Sitasahau adhabu kuamka alfajiri kwenda shule. Lazima nivuke mto, kunyeshewa mvua, kutembea umbali mrefu wa kilomita 19 kwenda kusoma sekondari ya kata jirani ya Sukuma. Ilikuwa kazi ngumu, ukijumlisha safari ya kwenda shule na kurudi nyumbani ni sawa na kutembea kilomita 38," anaeleza.

Ni hatua mpya inayompa tabasamu, shule kuwa karibu, akiwa mtoto wa kike anapata fursa sasa ya kusoma kwa bidii bila ya kukata tamaa aweze kutimiza ndoto zake kielimu, huku akiwashukuru wazazi na serikali kwa zawadi iliyowakomboa.



Mwenye fulana nyekundu, ni Diwani wa Kata ya Buhumbi, Petro Matonange na kulia kwake, mwenye suti za bluu ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Magu, Lutengano Mwalwiba, akikata utepe kuashiria ufunguzi wa shule hiyo. **PICHA ZOTE: ANTHONY GERVAS.**

# Zoé Kabila atimuliwa mamlakani

**Kinshasa, DRC**

ZOÈ Kabila, mdogo wa rais wa zamani wa DRC, Joseph Kabila, amefukuzwa kwenye nafasi ya gavana wa mkoa wa Tanganyika.

Wengi mwa wabunge walipiga kura ya kutokuwa na imani naye.

Ingawa baadhi wamepinga hatua hiyo, akidai kwamba haikufuata sheria.

Vyanzo vya RFI, vilisema Zoé Kabila Mwanzambala bado yuko Kinshasa, akizuiliwa na Wizara ya Mambo ya Ndani.

Kukosekana kwake katika mkoa wa Tanganyika, hakuna mjumbe wa serikali yake aliyetaka kushiriki katika mkutano huo kujibu mashtaka yaliyomo katika hoja ya kutokuwa na imani naye.

Katika sehemu kulikofanyika mkutano huo, walikuwapo wabunge 13 tu ambao walitoa hoja hiyo na ambao wanalaani usimamizi mbaya, ubadhirifu na ukosefu wa uongozi.

Hoja hii iliwasilishwa Jumanne wiki hii, kwa ajili ya mjadala uliyopangwa kufanyika juzi.

Wabunge wengine 12 wa Bunge la Mkoa walisusia mkutano huo, wakisema kwamba walikuwa wanajua matokeo.

Mkakati uliowekwa kwa matumaini ya kubatilisha hatua ya kutimuliwa gavana Zoé Kabila na timu yake, alisema mmoja wa wajumbe wa tawi la kundi la AFDC-A wanaoendelea kumuunga mkono rais mpya wa Seneti, Modeste Bahati Lukwebo, mwanachama wa Muungano mtakatifu wa taifa kutoka kambi ya Rais wa sasa, Félix Thisekedi.

Kwa upande wa Mbunge Claudel Lubaya na mawaziri wa zamani Marie-Ange Mushobekwa na Geneviève Inagosi, walisema sheria haijaheshimiwa.

Kwa sasa wanasubiri uamuzi wa Mahakama ya Katiba, ambayo inatarajia kutoa uamuzi kuhusiana na kesi hiyo.

**RFI**



Wafanyakazi wa matanuri ya kuchomea maiti wakiwa wameelemewa na wimbi kubwa la watu wanaohitaji huduma hiyo kwa wapendwa wao waliofariki kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa corona nchini India jana. **(PICHA: AFP)**

# Kenya kufanya sensa ya kwanza wanyamapori

**Nairobi, KENYA**

KENYA kwa mara ya kwanza, mamlaka imezindua sensa ya wanyamapori.

Uzinduzi huo umefanyika rasmi Mashariki mwa Kenya katika Hifadhi ya Taifa ya Milima ya Shimba.

Mamlaka ya Wanyamapori (KWS), ilisema sensa ya wanyama wa porini kitaifa, imelenga kupata jumla ya idadi ya wanyamapori na eneo walipo.

"Zoezi hili litabainisha idadi ya wanyamapori waliopo na kutambua vitisho vilivyowakabili katika hifadhi," huduma ya wanyamapori ilieleza.

KWS inashirikiana na watafiti wa wanyamapori na taasisi ya mafunzo huru, ambayo inafanya utafiti wa hifadhi za wanyama hao na wanaowasimamia.

Kenya ina hifadhi za wanyamapori katika maeneo mbalimbali ya nchi.

**BBC**

## Malkia wa Zulu azikwa, mrithi wake bado asakwa

**KwaZulu-Natal,** AFRIKA KUSINI

MALKIA Mantfombi Dlamini Zulu wa jamii ya Zulu nchini Afrika Kusini amezikwa.

Mazishi yake yalifanyika katika kasri lake la Kwakhangelamankengane, mjini Nongoma nyakati za alfajiri.

Ukumbusho wake ulifanyika usiku kucha.

Alizikwa kulingana na utamaduni wa ufalme wa WaSwati.

Mwili wa malkia ulifungwa kwa ngozi ya ng'ombe ambayo ulipewa ujumbe uliotumwa na kaka yake, Mfalme Mswati III wa Eswatini.

Mazishi yalihudhuriwa na jamaa zake kutoka pande zote mbili za ufalme.

Shughuli ya kumuaga rasmi iliyofadhiliwa na serikali ilifanyika baadaye jana.

Baada ya Malkia Mantfombi kuzikwa, kilichosalia ni kumtafuta atakayeongoza ufalme wa Zulu.

**BBC**

## Ethiopia yapewa dola milioni 65

**Addis Ababa,** ETHIOPIA

UMOJA wa Mataifa ((UN), umetoa dola milioni 65 kwa mahitaji ya kibinadamu nchini Ethiopia.

Kati ya hizo dola milioni 40, zitakwenda kwenye operesheni ya msaada katika eneo la Kaskazini katika mkoa wa Tigray.

"Hali ya Waethiopia na maisha kwa jumla yanaharibiwa na ukame na watoto wanaugua utapiamlo," Mkuu wa Misaada ya UN, Mark Lowcock, alisema katika taarifa yake.

Alhamisi wakati wa kutangazwa kutolewa kwa fedha hizo.

"Na miezi sita katika vita huko Tigray, raia wanaendelea kubeba mzigo mkubwa.

"Wanawake na wasichana walengwa na unyanyasaji wa kijinsia na mamilioni wanateseka kupata huduma muhimu na chakula, haswa katika maeneo ya vijijini ambayo hayawezi kufikiwa kabisa."

Alisema majibu ya kibinadamu yanahitaji kuongezwa sasa na kwamba zaidi ya watu milioni 16 wanahitaji msaada kote nchini Ethiopia, pamoja na wastani wa milioni 4.5 katika mkoa wa Tigray.

Tigray imekuwa kitovu cha uhasama tangu Novemba, wakati mapigano yalipozuka kati ya Tigray People's Liberation Front (TPLF) na ya serikali ya Waziri Mkuu wa Ethiopia, Abiy Ahmed.

Maelfu ya wakazi wa Tigray wamekimbilia Sudan kutoroka mapigano.

**VOA**

## Mwanahabari afungwa kwa ugaidi

**Kigali,** RWANDA

MAHAKAMA ya Rwanda imemhukumu mwandishi wa habari, Phocas Ndayizera na wengine sita kifungo cha miaka 10 gerezani kwa mashtaka ya ugaidi.

Wamekutwa na hatia kwa kosa la kupanga kulipua eneo la umma katika mji mkuu wa Kigali na kula njama za kufanya ugaidi.

Jaji alisema mahakama ingeweza kuwapa kifungo cha miaka 20 na 25 lakini wamepewa miaka 10 kwasababu mpango wao haukufanikiwa na hivyo haukusababisha athari kwa umma.

Katika mkutano wa kwenye video uliofanyika juzi mchana, wengine sita mahakama iliamuru waachiwe huru kwa mashtaka yanayowakabili.

Novemba mwaka 2018, mwandishi Ndayizera alipotea kwa siku saba, kabla ya kufikishwa polisi wiki moja baadaye wakati walipokamatwa kwa makosa ya kufanya mpango wa shambulio la mlipuko. Ndayizera na wenzake wamekanusha mashtaka hayo yote.

**BBC**

## 25 wauawa operesheni ya dawa za kulevya

**Rio de Janeiro,** BRAZIL

TAKRIBANI watu 25, ikiwa pamoja na ofisa wa polisi, waliuawa juzi katika operesheni kubwa dhidi ya dawa za kulevya katika eneo moja lililoko Rio de Janeiro.

Taarifa za vyombo vya habari vya Brazil viliripoti.

Operesheni hiyo ilifanywa dhidi ya wafanyabiashara wa dawa za kulevya wanaotuhumiwa kuajiri watoto wadogo katika kitongoji duni cha Jacarezinho, Kaskazini mwa mji wa Rio, tovuti ya habari ya G1 imeripoti, ikinukuu polisi. Televisheni ya GloboNews, ilirusha hewani picha zinazoonyesha watu wenye silaha wakikimbia wakati wa operesheni ya polisi.

Wakazi pia walikuwa wakirusha video kwenye mitandao ya kijamii zinazoonyesha milipuko, milio ya risasi na helikopta zikiruka juu ya eneo hilo.

Watu walalamikia ukatili uliofanywa, idadi kubwa ya polisi walionekana wakizunguka kitongoji hicho.

Wakazi walisikia milio ya risasi kutoka pande zote huku kukiwa na hofu kubwa, kama alivyosema wakili wa haki za binadamu, Maria Julia Miranda akiongea na mwandishi wa RFI, Martin Bernard.

"Huu ni ugaidi kabisa katika eneo hili. Jambo la kwanza linaloumiza ni kiwango cha damu unachoweza kuona katika eneo hili, kulionekana damu nyingi zikitapakaa ardhini.

"Katika nyumba ya kwanza tuliyotembelea, familia ilifukuzwa, kijana mmoja aliuawa katika chumba cha kulala cha msichana wa miaka minane.

"Familia iliona ukatili huu. Mtoto huyu ameumizwa sana na kitendo hiki cha kikatili."


Ofisa wa polisi aliuawa katika operesheni hiyo, ingawa watu wengine waliouawa hawakutajwa.

"Leo, tunaona ushahidi wa tisa, kwa mara nyingine tena, kwamba hakuna sheria katika vitongoji vya Rio", alisema Joel Luiz da Costa, mtu anayesimamia Taasisi ya Ulinzi ya watu Weusi.

**RFI**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**WILLIAM RUGUMAMU** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye index namba H439/542/1969 kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary SHINYANGA mwaka 1969,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi

**Polisi taarifa**
**DAR/CHU/RB/235980/2021**

## KUPOTEA KWA CHETI



**CHRISTINE F. TASIA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.2499-0013 kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia TUSIIME SEKONDARI November, 2013. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya **Polisi: DAR/OST/RB/233994/2021.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**BONIFACE B. MAGAYANE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha sita chenye index namba S0132-0806 kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2010 katika shule ya Milambo High School mwaka 2010. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi **Taarifa: KIG/KIG/RB/233032/2021.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**ANISIA DOMINICK MIRENYI** anatangaza kupotelewa na cheti cha chuo chenye namba **T/DEG/2015/0064** kilichotolewa na Chuo kikuu cha Mwenge Catholic(MWECAU) kuanzia mwaka **2015- 2018** cha Bachelor of science in Mathematics and Statistics.
Yeyote atakayekiokota atoe taarifa Kituo chochote cha polisi.
Taarifa ya polisi: **MAN/BAB/RB/375231/2020**

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**
**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**MIRATHI NA 16 YA MWAKA 2021**
**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**
**DOROTHY AUGUSTINO WANZALA**
**MWOMBAJI/WAOMBAJI**
**RENATUS AUGUSTINE WANZALA**
**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa waomba-ji/mwombaji hapo juu.
Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo Dar Es Salaam ,leo tarehe 29 mwezi wa APRIL mwaka 2021.

NAIBU MSAJILI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Baruapepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaawa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA
Tarehe 07-05-2021

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya JUMATANO tarehe 12-05-2021 Kampuni ya FAMARI INVESTMENT itasafirisha Mzigo wenye vipimo vikubwa kutoka DAR ES SALAAM kuelekea TUNDUMA gari hilo lenye namba za usajili **T 860 DJT / T 937 AMF**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| Urefu | - | mita | 21 |
| Upana | - | mita | 3.1 |
| Kimo | - | mita | 5.2 |

3. Njia itakayotumika: DAR ES SALAAM hadi TUNDUMA kupitia VIGWAZA/-MAKAMBAKO

Gari itasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Baruapepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaawa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA
Tarehe 07-05-2021

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya JUMATANO tarehe 12-05-2021 Kampuni ya FAMARI INVESTMENT itasafirisha Mzigo wenye vipimo vikubwa kutoka DAR ES SALAAM kuelekea TUNDUMA gari hilo lenye namba za usajili **T 368 DDS/ T 907 DDB**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| Urefu | - | mita | 21 |
| Upana | - | mita | 3.1 |
| Kimo | - | mita | 5.2 |

3. Njia itakayotumika: DAR ES SALAAM hadi TUNDUMA kupitia VIGWAZA/-MAKAMBAKO

Gari itasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Baruapepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaawa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA
Tarehe 07-05-2021

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya JUMATANO tarehe 12-05-2021 Kampuni ya FAMARI INVESTMENT itasafirisha Mzigo wenye vipimo vikubwa kutoka DAR ES SALAAM kuelekea TUNDUMA gari hilo lenye namba za usajili T 850 DJT / T 515 AKU
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| Urefu | - | mita | 21 |
| Upana | - | mita | 3.1 |
| Kimo | - | mita | 5.2 |

3. Njia itakayotumika: DAR ES SALAAM hadi TUNDUMA kupitia VIGWAZA/-MAKAMBAKO

Gari itasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Baruapepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaawa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA
Tarehe 07-05-2021

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya JUMATANO tarehe 12-05-2021 Kampuni ya FAMARI INVESTMENT itasafirisha Mzigo wenye vipimo vikubwa kutoka DAR ES SALAAM kuelekea TUNDUMA gari hilo lenye namba za usajili **T 376 DDS / T 209 ARC**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| Urefu | - | mita | 21 |
| Upana | - | mita | 3.1 |
| Kimo | - | mita | 5.2 |

3. Njia itakayotumika: DAR ES SALAAM hadi TUNDUMA kupitia VIGWAZA/-MAKAMBAKO

Gari itasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Baruapepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaawa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA
Tarehe 07-05-2021

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya JUMATANO tarehe 12-05-2021 Kampuni ya FAMARI INVESTMENT itasafirisha Mzigo wenye vipimo vikubwa kutoka DAR ES SALAAM kuelekea TUNDUMA gari hilo lenye namba za usajili **T 378 DJY / T 944 ABK**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| Urefu | - | mita | 21 |
| Upana | - | mita | 3.1 |
| Kimo | - | mita | 5.2 |

3. Njia itakayotumika: DAR ES SALAAM hadi TUNDUMA kupitia VIGWAZA/-MAKAMBAKO

Gari itasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

NASSER ADAM KINGU ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI T 130 DJN – TOYOTA BREVIS. CHASSIS NAMBA JCG10-0056043. YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: DAR/KIJ/RB/236463/2021.

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**
**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**MIRATHI Na. 20 YA MWAKA 2021**
**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**
**THE LATE: AL-HASSAN ALLY BWANGA WAOMBAJI**
**MWANAARABU MOHAMED TALLE NA ASHURA ALLY BWANGA**
**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa Mirathi kwa waombaji/mwombaji hapo juu. Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 7th Mwezi wa June, 2021.
Imewasilishwa Dar es salaam, leo tarehe 6 Mwezi wa May, 2021.

NAIBU MSAJILI




OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

MWANZONI ilionekana ni fahari. Wazazi kupata mtoto wa kike. Akaja kuwa msichana mzuri aliyeumbwa akaumbika na kutamaniwa na kila mtu, ni sifa kubwa. Wakati mwingine mzazi hupata hata vizawadi vidogo kutoka kwa watu mbalimbali bila kujua kuwa nia ni kutengeneza mazingira kwa binti yao. Kinyume chake mzee Ngoma na mkewe Fatuma wanapata mtoto wa kike Bishada ambaye anaondokea kuwa tishio kwenye kijiji cha Mtakuja kwa urembo wake.

Badala ya kuwa tija na faraha kwa wazazi wake anageuka kuwa balaa. Wazazi wanakuwa hawana amani kutokana na vitisho mbalimbali ikiwemo kuuawa kutoka kwa watu mbalimbali ndani na nje ya kijiji hicho. Inakuwa tafrani. Kijiji hakikaliki. watu wanatafutana. Moto unawaka. Bishada mwenyewe maisha yake yanakuwa hatarini. Fuatilia kisa hiki ambacho kitakuacha mdomo wazi.

# Aolewe au afe-**5**

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**

**Na Adam Fungamwango**

WANAUME na vijana baadhi yao nao waliingia kwenye kundi la kumchukia msichana huyo kwa sababu pamoja na jitihada zote za kumtongoza, angalau tu kutembea naye, lakini Bishada alikuwa na msimamo thabiti usioyumba.

Achia mbali wale waliopeleka barua za uchumba na zikadunda, ukichanganya, Bishada alikuwa na maadui wengi kuliko alivyodhani.

"Haya wanakijiji, tumepata picha halisi ya msichana huyu jinsi alivyo. Pamoja upole wote kumbe ni mhuni tu. Na hii yote ni kwa sababu hajaolewa. Sasa mimi kama Mwenyekiti. Kabla ya watu kutoa ushuhuda, tulikaa na kamati yangu. Tumeamua kitu kimoja. Tumetoa mwezi mmoja huyu binti awe ameshaolewa au kuposwa ili matatizo yote haya yasiwepo. Vinginevyo mzee Ngoma, mkeo Bi Fatuma tutawafukuza kwenye kijiji hiki." Alisema Mwenyekiti na kufuatiwa na mayowe, vigelegele na makofi.

"Hatufanyi hivi kwa sababu hatumpendi binti au mzee Ngoma, ila tunataka kijiji chetu kirudi kwenye hali ya amani na utulivu. Akiwa ameolewa au kuposwa, hata kama akiwa hapa hapa kijijini, atakuwa tayari yupo kwenye himaya na uangalizi wa mtu, kuliko hivi sasa yupo huru, basi kila mtu macho kwake." Alihitimisha Mwenyekiti na kufunga mkutano huo.

Ni mkutano ambao ulikuwa mwiba kwa familia ya Bishada, lakini ni faraja kwa wale wote ambao walishawahi kupeleka barua za posa kwa kina Bishada.

Sasa walijua bahati imekuja tena. Walijua safari hii hazitokataliwa tena kama mwanzo. Zaidi ya barua 15 zili薬letwa nyumbani kwa mzee Ngoma, lakini Bishada alikataa katakata.

Kwa wanawake wao hawakuwa na shida. Walijua Bishada akichumbiwa kwao itakuwa ni nafuu kwenye ndoa zao, au kwa wapenzi wao.

Kazi ilikuwa kwa wanaume. Kila mmoja alijua hata kama Bishada akikubali, lakini barua au posa itakayokubaliwa ni moja tu. Sasa ni nani atakubaliwa?

Mzee Ngoma, mkewe Bi. Fatuma na binti yao Bishada walikuwepo kwenye kikao hicho. Ilikuwa ni aibu kubwa kwao. Mzee Ngoma na mkewe walijua wazi kuwa ulikuwa ni uongo wa wazi ulitungwa.




Wanamfahamu binti yao. Wanafahamu msimamo wake. Pamoja na kwamba hawakumuunga mkono kitendo chake cha kukataa wanaume, lakini walisimama upande wake kupinga uongo wote juu yake.

Bishada alilia wiki nzima. Alikaa ndani tu. Hata kula alikataa. Alikuwa akibembelezwa na mama yake na shoga yake Mariam.

******************************

Alikuwa amekonda. Si Bishada yote. Kama si juhudi za baadhi ya ndugu zake, pamoja na majirani wachache wanaoihurumia familia hiyo bado angeendelea kuwa ndani. Na angeendelea kukataa kula.

Ilianza kujisikia vizuri, ingawa siyo sana. Alikuwa na siku tatu tu ambazo alikuwa ameanza kula. Alichukua ndoo yake kwa nia ya kwenda kisimani. Alikuwa amekumbuka kisimani na kutembea pia.

"Utaweza kwenda kutoka na ndoo kisimani hadi hapa, maana nakuona bado afya yako siyo nzuri."

"Nitaweza mama."

Jibu hilo lilimfariji mama Bishada.

Naye pia hakuwa kwenye wakati mzuri, binti yake alipokuwa ndani kama mgonjwa.

Mwanzo aliona kuzaa binti mzuri kama Bishada ni tunu, lakini sasa anaona kama ni balaa.

Kufukuzwa kijijini, kuchukiwa na kila aina ya matatizo wanayoyapata ni kwa sababu ya Bishada.

Na hakuna kosa lolote analofanya, ila ni kukataa tu kuolewa na wanaume wanaokuja kutaka kumposa na wengine tu ambao wanamtaka kimapenzi.

Alitembea taratibu kuelekea kisimani. Kwa mbali aliona kama kitu cheupe katikati ya njia.

Kwanza alisita. Lakini akakifananisha na kitu kama karatasi. Akaanza kusogea taratibu kuona kama ni yenyewe. "Ndiyo, ni karatasi." Alijisemea mwenyewe alipofika hatua tano kutoka kwenye kitu hicho.

Bado hakujua kama ilimdondoka mtu aliyekuwa anapita au imewekwa hapo kwa makusudi.

Licha ya matatizo yote ya kijijini hapo na hata vya jirani, hakudhani kama inaweza ni kitu cha kutegwa yeye ili adhurike.

Alidhani tu kuna mtu alidondosha karatasi. Aliweka ndoo chini na kuinama na uangalifu. Akaiokota. Ilikuwa imefungwa. Taratibu aliifungua. Hakukuwa na kitu chochote ndani. Si pesa, wala kitu kilichowekwa ndani ya karatasi zaidi ya maandishi.

Aliisoma hadi mwisho. Akairudia tena. Mapigo ya moyo yalianza kumuenda mbio.

Aliikunja karatasi ile na kuifunga kwenye fundo ya kanga ambayo alitaka kuitumia kama ngata kwa ajili ya kubebea ndoo ya maji.

Aliinua ndoo yake na kurejea kwa haraka pamoja na woga, akitazama huku na huko. Jinsi alivyoisoma karatasi ile alijua kabisa iliwekwa makusudi na si kwa bahati mbaya. Ilimlenga yeye. Ina maana aliyoiweka alikuwa ama anamuona alipokuwa anakuja hadi anaisoma barua ile, au alijua atapita hapo muda si mrefu. Kwa maana hiyo alijua anaangalia na chochote kibaya kinaweza kutokea.

**Alidhani tu kuna mtu alidondosha karatasi. Aliweka ndoo chini na kuinama na uangalifu. Akaiokota. Ilikuwa imefungwa. Taratibu aliifungua. Hakukuwa na kitu chochote ndani.**

Alipofika karibu na nyumbani alitimua mbio. Alifika nyumbani akiwa hoi, mkononi akiwa na ndoo bila maji.

Mama yake alishtuka na kushangaa kwa wakati mmoja.

"Nini wewe?"

Hakujibiwa.

"Nyoka?"

Bishada alifungua fundo kwenye khanga na kumpa mama yake karatasi ile.

"Bishada Binti Ngoma. Uzuri wako usifanye fimbo ya kutupigia sisi wanaume. Najua baada ya ule mkutano utakubali moja ya barua zitakazokuja. Naitwa mzee Buntungwa, nadhani unanifahamu. Kesho tunatuma mshenga kwa ajili ya kijana wangu Limiko. Hiyo ndiyo uikubali. Vinginevyo unajitafutia matatizo. Kwa hiyo una mawili tu ya kuchagua. Ukubali barua ya kijana wangu Limoko ili uishi. Au ukatae ufe. Ndiyo utakufa na najua mimi mbinu nitakayotumia ili kukuondoa hapa duniani. Kumbuka kuwa hata ukimkubali mtu yoyote na kumkataa Limiko, kifo ni halali yako. Na kwa sababu kijiji kimeshawachoka wewe na familia yako, huwezi kwenda kushtaki popote juu ya kutishia ukasikilizwa. Uamuzi sasa unao mwenyewe, ahsante."

Mama hakuamini alichokuwa akikisoma. Bishada aliingia chumbani kwake na akuanza kuangua kilio.

Akili yake moja kwa moja ikamtuma kuwa kilichobaki wahame tu kijiji hicho. Watoke hapo waende wakajiandikishe kwenye kijiji chochote cha mbali. Huku watakachobakisha ni ardhi yao na mashamba tu. Hali hiyo ilishaanza kumchosha. Ni kweli alikuwa akigombana mara kwa mara na binti yake juu ya kutotaka kuolewa. Lakini hii ya kulazimisha na kutaka kumuua Bishada ilimfikirisha na kumtisha. Aliona kabisa kilichobaki wanamuulia tu binti yake ili wakose wote. Hakuonekana ana dalili za kumkubali mwanaume yoyote yule.

Kabla ya uamuzi wote huo ambao ulikuwa unamsubiria mzee Ngoma arejee aliingia chumbani kwa binti yake na kumkuta machozi yalimtoka akiwa amejikunyata.

"Mama, kwani kuolewa ni lazima au hiari?" Aliuliza kwa uchungu.

"Hiari mwanangu." Alijibu kwa uangalifu.

"Sasa mbona mimi nalazimishwa. Huyu anataka eti nimkubali kijana wake Limiko. Hata kama nikikubali kwa sababu ya kuogopa kuuawa, itakuwa ni ndoa au utumwa?" Alihoji Bishada kwa hasira kana kwamba mama yake ndiyo anayemlazimisha.

ITANEDELEA JUMAMOSI

# BEI YA SANCHO YAWEKWA HADHARANI




**DORTMUND,** Ujerumani

KLABU ya Borussia Dortmund wameamua kushusha bei yao ya mauzo kwa winga wa Timu ya Taifa ya England, Jadon Sancho kufikia paundi milioni 78.

Vyombo mbalimbali vya habari nchini Ujerumani, vimeripoti kuwa kipengele cha Sancho cha awali cha kuondoka kwa dau la pauni milioni 108 kimeshushwa.

"Tayari tulikuwa na makubaliano na Jadon mwaka jana kwamba, anaweza kubadilisha kipengele fulani," amenukuliwa Michael Zorc Mkurugenzi wa Soka wa Dortmund na mtandao wa ARD.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, ambaye ameona timu nyingi zikipunguza mapenzi naye, anafikiria hatua inayofuata na kuna uwezekano wa kuondoka mwishoni mwa msimu huu.

Sancho kwa sasa hayupo kwenye kiwango sawa kama mshambuliaji mwenzake, Erling Haaland na ingawa klabu hiyo ya Ujerumani inatarajia kuwabakisha wachezaji wote wawili.

Baada ya sakata la msimu uliopita wa majira ya joto kuihusisha Manchester United, wengi wanatarajia kikosi cha Ole Gunnar Solskjaer kitarudi na ofa mpya kwa fowadi huyo msimu wa joto.

# Sarri atajwa kutua Tottenham

**LONDON,** England

KLABU ya Tottenham Hotspur imeripotiwa kumtambua Maurizio Sarri kama chaguo lao la kwanza kuchukua nafasi ya Jose Mourinho kama kocha mkuu wa timu hiyo.


Ryan Mason kwa sasa anasimamia klabu kwa muda wakati wana London Kaskazini hao wakitafuta mbadala wa muda mrefu wa Mourinho, ambaye alifutwa kazi mwezi uliopita.

Ripoti ya hivi karibuni ilidai kwamba Spurs ilikutana na Antonio Conte wa Inter Milan kuzungumzia jukumu la usimamizi katika klabu, wakati majina mengine kadhaa yamehusishwa na nafasi hiyo.

Kwa mujibu wa Calciomercato, Tottenham wanamuona Sarri kama "chaguo la kwanza" kuwa kocha mkuu mpya wa timu mwanzoni mwa msimu wa 2021-22.

Ripoti hiyo inadai kuwa Roma walipendezwa na kocha huyo mwenye umri wa miaka 62 kabla ya kumthibitisha Mourinho na sasa mawasiliano tayari yamefanywa kati ya Spurs na Mtaliano huyo.

Sarri, ambaye amekuwa nje ya kazi tangu kufutwa kazi na Juventus Agosti iliyopita, aliiongoza Chelsea wakati wa msimu wa 2018-19 kutwaa taji la Ligi ya Europa na fainali ya Kombe la EFL.






# *Aguero aanza kuteta na Barcelona*

**MANCHESTER,** England

BARCELONA wameanza mazungumzo ya kumsajili mshambuliaji wa Manchester City, Sergio Aguero, kwa mujibu wa Sky Sports.

Barca wanataka kuimarisha safu yao ya ushambuliaji kwa ajili ya msimu ujao na wanawania kumsajili Aguero kipindi cha majira ya joto kinachokuja.

Mshambuliaji huyo raia wa Argentina atakuwa mchezaji huru katika msimu wa joto, wakati mkataba wake pale kwenye dimba la Etihad utakapomalizika na Camp Nou sasa wanazungumza naye juu ya kumhamishia Hispania.

Aguero ataondoka City akiwa mfungaji bora wa muda wote katika klabu hiyo akiwa amefunga mabao 257 katika mashindano hayo tangu atue hapo Etihad miaka 10 iliyopita.

Mshambuliaji huyo anataka kushinda Ligi ya Mabingwa Ulaya kabla ya kujiunga na Barcelona, taji ambalo amelikosa katika kipindi chote alichocheza pale Etihad.

## HABARI MICHEZO

# PSG yajiandaa kumsajili Mo Salah

**PARIS,** Ufaransa

PARIS Saint-Germain inaripotiwa inataka kujaribu kumsajili mshambuliaji wa Liverpool, Mohamed Salah, kama Kylian Mbappe ataondoka klabuni hapo.


Mbappe bado hajasaini mkataba mpya na mabingwa hao wa Ufaransa, na mshambuliaji huyo anatarajiwa kuuzwa katika soko lijalo ikiwa hatasaini mkataba mpya.

Real Madrid inaendelea kuhusishwa sana na mshindi huyo wa Kombe la Dunia, ambaye amebakiza miezi 12 kukamilisha mkataba wake wa sasa hapo jijini Paris.

Kwa mujibu wa Le Parisien, PSG inafanya mipango ya dharura iwapo mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa ataondoka klabuni hapo, na klabu ikimtambua Salah wa Liverpool kama mbadala.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Misri, ambaye anatajwa kuwavutia Real Madrid na Barcelona, hivi karibuni alibainisha kwamba Liverpool bado hawajajaribu kuzungumza naye juu ya mkataba mpya.

Salah kwa mara nyingine, amekuwa katika kiwango cha kuvutia pale Liverpool msimu huu licha ya panda shuka ya timu hiyo, akifunga mabao 29 katika mechi 46 za mashindano yote, ikiwa ni pamoja na mabao 20 katika michezo 32 ya Ligi Kuu England.





# RONALDO KUTOREJEA TENA MAN UNITED

**TURIN,** Italia

CRISTIANO Ronaldo ameripotiwa hatajiunga tena na Manchester United kipindi cha majira ya joto, kwani mabingwa hao wa mara 20 wa Ligi Kuu England hawawezi kumsajili mshambuliaji huyo wa Juventus.

Hatima ya nyota huyo wa Ureno kule Turin kwa sasa ipo mashakani wakati kuna maoni kwamba, anazidi kuchanganyikiwa na maisha katika klabu yake hiyo ya Italia. Kurejea United kulitajwa kuwapo katika uwezekano wa mpango wa uhamisho, na Mashetani Wekundu hao wakidhaniwa wako tayari na wazo la kumrudisha Old Trafford nyota wao wa zamani mwenye umri wa miaka 36 katika soko lijalo.

Hata hivyo, kwa mujibu wa Sport Mediaset, upande wa Ole Gunnar Solskjaer hautaweza kumudu dau la jumla la Ronaldo, ambaye anaaminika kulipwa pauni 540,000 kwa wiki huko Turin, wakati kibibi kizee hicho cha Turin kikidai dau kubwa la uhamisho.

Ripoti hiyo inadai kwamba, raia huyo wa Ureno anajiandaa kuona mwaka wa mwisho wa mkataba wake wa Juve kabla ya kutafuta klabu nyingine mwishoni mwa msimu wa 2021-22. Ronaldo, ambaye amefunga mabao 34 katika mechi 40 kwa kikosi cha Andrea Pirlo msimu huu, pia kwa sasa anahusishwa na kurudi Sporting Lisbon.

# Bayern, Arsenal zamgombea Hakimi

**MUNICH,** Ujerumani

BAYERN Munich wameripotiwa kuwa tayari kupambana na Arsenal sokoni kuwania saini ya beki wa Inter Milan, Achraf Hakimi.

Huku Hector Bellerin akionekana kuwa amepanga kutafuta klabu mpya msimu ujao, Arsenal wanadhaniwa wamemwainisha Hakimi kama chaguo bora kwa beki wa kulia.


Nyota huyo wa zamani wa Real Madrid amekuwa sehemu ya muhimu ya kwa Inter wakati ikitwaa taji la Serie A msimu huu - akifunga mabao saba na kutoa usaidizi kwenye mengine saba katika mechi 33 za Ligi Kuu England.

Sasa, mwandishi wa habari wa Ujerumani, Manuel Bonke amedai kwamba, kocha mpya wa Bayern, Julian Nagelsmann amemtambua Hakimi kama mchezaji muhimu, lakini bei ya pauni milioni 50 inaweza kuleta shida. Hakimi hapo awali alisisitiza kuwa anafurahi kuwepo Inter, ambapo ana mkataba hadi mwaka 2025 baada ya kuwasili kutoka Real Madrid msimu uliopita wa majira ya joto.

Jitihada za kuwawinda Tariq Lamptey wa Brighton & Hove Albion na Max Aarons wa Norwich City pia zinatajwa kuwa kwenye mpango wa Arsenal, katika jitihada za kumtafuta beki mpya wa kulia.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# CAVANI AMEONYESHA KWANINI TUNATAKA ABAKI - SOLSKJAER

Kiwango cha juu anachokionyesha kinamfanya awe mchezaji muhimu anayetakiwa kuendelea...

**ROME,** Italia

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer amesema Edinson Cavani ameonyesha kwanini klabu inataka kumbakiza Old Trafford baada ya kuwaongoza mashetani wekundu hao kwenye fainali ya Kombe la Ligi ya Europa.

**Cavani alifunga mabao mawili katika ushindi wa 3-2 kwenye mchezo wa pili wa nusu fainali wa mashindano hayo wa ugenini dhidi ya Roma, Alhamisi, lakini United ilifuzu hatua hiyo kwa uwiano wa mabao 8-5.**

Nyota huyo wa United, Cavani, ambaye mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu huu 2020-21, alifunga katika kila kipindi kuwahakikisha miamba hao wa Ligi Kuu England kufuzu fainali ya kwanza chini ya kocha, Solskjaer.

Baada ya mabao mawili katika mchezo wa kwanza, Cavani sasa amekuwa mchezaji wa kwanza kufunga mabao zaidi ya mawili kwenye mechi mbili za nusu fainali kwenye mashindano makubwa Ulaya, tangu Klaus Allofs alipofanya hivyo kwenye Kombe la UEFA msimu wa 1985-86 akiwa na klabu ya Cologne.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34 raia wa Uruguay - alikuwa akihusishwa na kujiunga na Boca Juniors - amefunga mabao 16 katika mechi 15 zilizopita kwenye Ligi ya Europa, yakiwamo 15 katika mechi zake 10 alizoanza katika mashindano hayo.

Wakati United ikijaribu kumshawishi Cavani kuongeza mkataba wa kubaki Manchester, Solskjaer amemsifia mfungaji huyo wa wakati wote wa Paris Saint-Germain.

"Edinson ameonyesha tena kwanini tunataka kumbakiza Old Trafford," alisema Solskjaer akiwaambia waandishi wa habari, wakati United sasa inasubiri kucheza fainali hiyo Mei 26 dhidi ya Villarreal.

"Mpira wa miguu una lugha yake. Nafikiri Edinson amethibitisha hilo usiku wa leo (juzi), na katika mechi zilizopita, ingawa katika maisha yake ya soka amekuwa kifanya hivyo mara kwa mara."

United katika mechi wa kwanza ilishinda mabao 6-2 jijini Manchester, lakini hawakuwa kwenye kiwango bora zaidi kwenye mchezo wa juzi hapa dhidi ya Roma.

## ZISIKUPITE

### AGUERO YAMTAKA BARCA

BARCELONA wameanza mazungumzo na wawakilishi wa mshambuliaji wa Argentina, Sergio Aguero mwenye umri wa miaka 32, ambaye mkataba wake na Manchester City unamalizika msimu huu. ***(Sky Sports)***

### MATIC KUMFUATA MOURINHO

KUTEULIWA kwa Jose Mourinho kuwa kocha mpya wa AS Roma msimu ujao huenda kukamfanya kiungo wa kati wa Italia, Lorenzo Pellegrini (24), kuhamia Liverpool, baada ya kocha klabu hiyo kuonyesha nia ya kuwaleta wachezaji wapya, miongoni mwao akiwamo nyota wa kimataifa wa Serbia na Manchester United, Nemanja Matic (32). ***(Mirror)***

### DE GEA ANUKIA ROMA

JOSE Mourinho pia ana matumaini ya kuungana tena na kipa wa Manchester United na Hispania, David De Gea mwenye umri wa miaka 30, baada kuchukua usukani AS Roma. ***(Todofichajes)***

### NYOTA WAMHOFIA ZIDANE

WACHEZAJI wa Real Madrid wanahofia kocha wao, Zinedine Zidane mwenye umri wa miaka 48, "amechoka na kukasirika" na huenda akaondoka klabuni hapo kabla ya kukamilisha mwaka wa mwisho katika mkataba wake msimu huu wa joto. ***(Goal)***

### ARSENAL, SPURS VITANI

ARSENAL inaongoza katika mbio za kuwania kumsajili kiungo wa kati wa Brighton, Yves Bissouma mwenye umri wa miaka 24, huku Tottenham, West Ham na Everton pia zikimwania. ***(Express)***

### BISSOUMA ANUKIA CITY

MANCHESTER City wanatafakari uwezekano wa kumsajili mchezaji wa kimataifa wa Mali, Yves Bissouma mwenye umri wa miaka 24, baada ya kujiondoa katika kinyang'anyiro cha kumsaka, Declan Rice (22), kutoka West Ham. ***(Star)***

### BEI YA SILVA YATAJWA

MANCHESTER United wameambiwa mshambuliaji wa Eintracht Frankfurt, Andre Silva mwenye umri wa miaka 25 raia wa Ureno, anagharimu pauni milioni 35. ***(Express)***

### MABEKI CHELSEA SOKONI

CHELSEA itawauza walinzi wake kwa ajili ya kukusanya fedha za kuwanunua wachezaji wengine, wanaopigiwa upatu kuondoka Stamford Bridge ni Marcos Alonso mwenye miaka 30 na Emerson Palmieri (26). (Goal)

### PIUG AKARIBIA ATLETICO

ATLETICO Madrid wanamnyatia kiungo wa kati wa Barcelona mwenye umri wa miaka 21, Riqui Puig. ***(Fichajes)***

### HENRIQUE AGEUKA LULU

BARCELONA na Paris Saint-Germain wanamfuatilia mlinzi wa Monaco kutoka Brazil, Caio Henrique mwenye umri wa miaka 23. ***(UOL)***

HABARI MICHEZO

## Tanzania yatarajia makubwa Senegal

**Na Saada Akida**

UIMARA uliopo katika kikosi cha Timu ya Taifa ya Soka la ufukweni unamfanya Kocha Mkuu, Boniface Pawasa kuamini itaenda kufanya vyema katika fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika zitakazofanyika hivi karibuni jijini Dakar, Senegal.

Katika fainali hizo Tanzania imepangwa kundi moja na wenyeji Senegal, Uganda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Pawasa alisema wachezaji wake wameimarika zaidi na wamejiandaa kukutana na ushindani kuanzia hatua hiyo ya makundi.

Pawasa alisema anaendelea na programu zake mbalimbali ikiwamo kuwafundisha mbinu za kuwabana wapinzani wao, lakini akiimarisha ubora wa mchezaji mmoja mmoja pamoja na kuwaandaa kisaikolojia kabla ya kuelekea Senegal katika fainali hizo.

"TFF imeleta mtu wa saikolojia kwa ajili ya kuwaweka sawa wachezaji, kwa ajili ya kwenda kufanya vizuri katika fainali hizi, tunataka kupata matokeo mazuri mbele ya wapinzani wetu akiwamo mwenyeji wa michuano hii," alisema Pawassa.

## Hard Rock bado yaitaka Ligi Kuu

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

LICHA ya Ligi Kuu Zanzibar kukosa mdhamini, uongozi wa Hard Rock umeahidi wataendelea kupambana hadi katika mchezo wake wa mwisho ili wajinusuru na janga la kushuka daraja.

Hard Rock inaburuza mkia katika msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar ikiwa na pointi 18, huku timu nyingine zilizoko kwenye hatari hiyo ni Chuoni yenye pointi 19 wakati bingwa mtetezi, Mlandege wapo katika nafasi ya 10.

Ligi hiyo itakayoendelea kuanzia Mei 22, mwaka huu itateremsha timu mbili msimu huu na klabu hizo zitaelekea katika Ligi Daraja la Kwanza Ngazi ya Kanda.

Kocha Mkuu wa Hard Rock, Ussi Ali Juma alisema bado ana matumaini timu yake itasalia kwenye ligi hiyo kama wachezaji wake watajituma na kuweka nia ya kuibakisha timu.

Juma alisema awali waliamini wameshaelekea pabaya lakini hesabu za kubakia katika ligi hiyo zilirejea baada ya kushinda mechi zake tatu mfululizo na hivyo wamepata nguvu mpya ya kupambana.

Alisema licha ya ligi hiyo kutokuwa na udhamini na kupelekea uendeshaji wake kuwa katika mazingira magumu, bado timu zimeendelea kuonyesha ushindani katika mechi zote wanazocheza.

Hard Rock yenye makazi yake Kisiwani Pemba imebakiza mechi tano ili kumaliza msimu huu na michezo hiyo yote itacheza ugenini Unguja.

# KMC YAAHIDI KUENDELEZA UBABE KWA AZAM FC BARA

**Na Saada Akida**

KOCHA MKuu wa KMC FC, Habib Kondo, amesema kikosi chake kimejipanga kuhakikisha kinachukuwa pointi tatu nyingine dhidi ya Azam FC kwa lengo la kujiimarisha katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo inaelekea ukingoni.

**Azam FC inatarajia kuikaribisha KMC katika mechi ya mzunguko wa pili itakayochezwa Mei 15, mwaka huu kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini Dar es Salaam.**

Akizungumza na gazeti hili jijini jana Kondo alisema anahitaji kupata ushindi katika mechi hiyo ili kukamilisha mipango yao ya kumaliza msimu huu wakiwa kwenye moja ya nafasi za nne za juu.

Kondo alisema kikosi chake kinaendelea vizuri na maandalizi ya michezo yote iliyopo mbele yao ikiwamo dhidi ya Azam FC na malengo yao ni kupambana ili kupata matokeo chanya.

Kocha huyo alisema walipata matokeo ya pointi tatu katika mchezo wa mzunguko wa kwanza uliochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru na sasa wanataka kufanya hivyo watakaporudiana licha ya kucheza ugenini.

"Malengo yetu kwa sasa ni kushinda mechi zilizopo mbele yetu na kuhitaji kumaliza katika nafasi ya nne za juu katika msimamo wa ligi, kwa sababu hiyo tutalazimika kupambana kuhakikisha tunashinda mechi zetu zote ili kufikia malengo hayo, ikiwa tunacheza nyumbani au ugenini," alisema Kondo.

Aliongeza wanaendelea kukiimarisha kikosi chao ili kiwe imara zaidi katika kila idara huku tayari ameyafanyia kazi mapungufu yaliyojitokeza kwenye michezo iliyopita.

Kocha huyo alisema hatua ya lala salama imekuwa na ushindani mkubwa kutokana na kila timu inahitaji matokeo mazuri ambapo baadhi wanapambana kuwania ubingwa, nafasi ya pili na wengine wanataka kujinasua na janga la kushuka daraja.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, KMC FC ambayo imecheza mechi 27 ina pointi 40 na iko katika nafasi ya tano wakati Azam FC yenye pointi 54, ikicheza mechi moja zaidi iko katika nafasi ya tatu.




Kocha Msaidizi wa Simba, Selemani Matola (kulia), akizungumza na waandishi mbalimbali wa habari kuhusiana na mchezo wa marudiano wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Yanga unaotarajiwa kuchezwa leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Morocco aahidi Namungo FC haishuki*

**Na Saada Akida**

HATUSHUKI. Ndio kauli ya Kocha Mkuu wa Namungo FC, Hemed Morocco kuelekea mwenendo wa kusuasua wa timu yake katika mechi za hatua ya lala salama katika Ligi Kuu Tanzania Bara.

Morocco aliliambia gazeti hili kazi kubwa ambayo anaifanya ni kupambana kuhakikisha wanapata matokeo mazuri katika michezo yao ya nyumbani ikiwamo dhidi ya KMC FC utakaochezwa wiki ijayo.

Kocha huyo alisema baada ya kupoteza pointi tatu dhidi ya JKT Tanzania, sasa anaelekeza nguvu zao katika kuhakikisha KMC hawaondoki na alama yoyote.

Aliongeza ligi hiyo imekuwa na ushindani kwa sababu hakuna timu ambayo ina uhakika kwa kufikia malengo iliyojiwekea, hivyo lolote linaweza kutokea endapo utazembea.

"Tumepoteza kiporo chetu dhidi ya JKT Tanzania, lakini tumejipanga vizuri kufanyia kazi mapungufu yetu na tuko tayari kuwakabili KMC FC, tunajua wapinzani wetu wako vizuri, kikubwa tunahitaji kupata pointi tatu kutoka kwao," alisema Morocco.

Alisema kutokana na ugumu uliopo katika ligi hiyo, wamejipanga kupambana ili kila mechi watakayocheza waondoke na matokeo chanya na kujiondoa kwenye nafasi ya hatari.

"Hatutabeza timu yoyote ambayo tutakutana nayo, tunatambua ubora wa KMC FC na tumejiandaa vizuri kupata matokeo mazuri kwenye mchezo huo na kujiweka katika mazingira mazuri ya kubaki katika Ligi Kuu kwa msimu mwingine tena," alisema Morocco.

# Michezo

Jumamosi Mei 8, 2021

Nipashe



Cavani ameonyesha kwanini abaki – Solskjaer UKURASA 22



Didier Gomes — Nesreddine Nabi

## 'Upepo huamua dabi'

**Na Adam Fungamwango**

BEKI wa zamani wa Yanga, Kenneth Mkapa amesema uzoefu wake katika mechi za watani wa jadi anaamini mara nyingi huamuliwa na hali ya mazingira yanayokuwapo na si kuangalia ubora wa vikosi vinavyokutana.

Akizungumza na gazeti hili, Mkapa alisema mechi hiyo ya leo itakuwa ngumu kama inavyokuwa kwenye 'dabi' nyingine zilizopita ingawa kila mmoja anajua kwa sasa Simba ipo vizuri zaidi.

Mkapa, beki huyo wa zamani wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), alisema anachofahamu ni kwamba wakati mwingine 'dabi' haimuliwi na ubora wa kikosi bali ni mazingira husika yanayokuwapo kwenye uwanja wakati huo.

Nyota huyo alikumbushia mechi yao dhidi ya Simba iliyochezwa mwaka 1988 ambapo Yanga ilitakiwa kutoa sare tu ili kutwaa ubingwa, lakini walikutana na kipigo cha mabao 2-1 kilichomnusuru Mnyama kushuka daraja.

"Ilikuwa mwaka 1988, mimi nilikuwa na msimu wa pili kwenye klabu ya Yanga na ilikuwa mechi ya nne dhidi ya Simba. Sisi Yanga tulikua vizuri sana, na tulihitaji siyo ushindi, ni sare tu ili tuwe mabingwa na Simba wao walihitaji ushindi na siyo sare ili kubaki Ligi Kuu. Vinginevyo walikuwa wanashuka daraja. Kwenye mechi hiyo Simba haikuwa vizuri sana, lakini tulifungwa mabao 2-1 na ubingwa tukaukosa, ukaenda kwa Coastal Union," alisema Mkapa.

Aliongeza wakati mwingine huku mechi ikiendelea uwanjani hutokea matukio ambayo huwatoa wachezaji mchezoni hasa timu ambayo iliyoonekana iko vizuri hali hugeuka lakini kwa tathmini yake kuelekea mchezo wa leo, timu itakayojipanga vizuri kimbinu, kiufundi na kisaikolojia ndiyo itakayoshinda.

# Watani kumaliza ubishi leo

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

### ●●● Tambo za makocha wa timu hizo zaendelea kutawala lakini 'Usiku wa deni'...

NCHI itasimama kwa dakika 90 ili kupisha mechi ya marudiano ya Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya watani wa jadi, Simba dhidi ya Yanga inayotarajiwa kuchezwa kuanzia saa 11:00 jioni leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

**Pamoja na utani wa jadi wa timu hizo mbili, lakini ni mechi ya leo pia inaweza kuamua mwelekeo wa kupata bingwa wa Tanzania Bara kwa msimu huu.**

Huu utakuwa mchezo wa 108 kuwakutanisha miamba hao, kwenye michezo 107 iliwakutanisha Yanga ni kinara akiwa ameshinda michezo 37, Simba akishinda mara 32 wakitoka sare mara 38.

Hata hivyo, vigogo hao watashuka dimbani wakiwa na kumbukumbu ya sare ya bao 1-1, ambayo walitoka katika mechi ya mzunguko wa kwanza.

Mechi hii itachezwa huku timu zote zikiwa na makocha wapya, ambao wote wametoka kwenye timu moja ya Al Merrikh ya Sudan, Didier Gomes wa Simba akiwa amevunja mkataba huku Nesreddine Nabi wa Yanga akitimuliwa baada ya kupata matokeo mabaya.

Akizungumza jijini jana, Kocha Msaidizi wa Simba, Selemani Matola, alisema wamejipanga kuonyesha mchezo safi, pamoja na kwamba ni mechi ngumu ya 'dabi', lakini hawatabadilisha falsafa yao.

Matola alisema wanahitaji kupata ushindi ili kuendelea kujiimarisha katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara na kuukaribia ubingwa wa msimu huu.

Alisema wanahitaji kushinda mechi zote za ligi zilizobakia ili kutimiza mipango yao ya kutetea ubingwa wa ligi pamoja na mashindano ya Kombe la FA ambayo pia wanashikilia taji lake.

"Hata kama ni 'dabi', tumejipanga kuonyesha soka safi la burudani, hatutaki kubutuabutua. Tunajua 'dabi' haijawahi kuwa rahisi, tunafahamu mchezo utakuwa mgumu lakini tumejiandaa kushinda na malengo yetu msimu huu ni kutetea ubingwa wa ligi," alisema Matola.

Kiungo na nahodha huyo wa zamani wa Wekundu wa Msimbazi alisema wachezaji wake wote wapo tayari kwa ajili ya mchezo huo na hakuna majeruhi hata mmoja katika kikosi chao au mwenye adhabu ya kadi.

"Tunaenda kucheza soka letu la kutafuta ushindi lakini pamoja na kuwapa burudani mashabiki watakaokuja kutusapoti uwanjani," alisema Matola.

Kocha wa Yanga, Nabi alikiri Simba ina kikosi kizuri msimu huu, anaiheshimu, lakini pia ina mapungufu yake ambayo anayafahamu huku pia hawaihofii.

"Tunajua Simba ni timu nzuri na ipo kwenye kiwango bora kwa sasa. Nampongeza kocha Gomes kwa kuifanya timu hiyo kucheza soka safi ndani na hata katika Ligi ya Mabingwa Afrika, hii inatoa taswira nzuri ya soka la Tanzania. Pamoja na yote ina mapungufu yake. Tunajua mchezo utakuwa mgumu, lakini tumejiandaa kushinda na hatuihofii," alisema Nabi.

Kocha huyo raia wa Tunisia aliongeza anawaheshimu Simba na anafahamu ubora wa Gomes huku akitarajia mchezo mzuri kutoka kwa pande zote mbili.

Naye nahodha wa Yanga, Haruna Niyonzima alisema mechi hiyo itakuwa nzuri na ngumu, lakini siku zote mechi kubwa huchezwa na wachezaji wakubwa.

"Tunaamini tutapambana kusaka ushindi, kila mchezaji amejiandaa kutimiza majukumu yake katika mechi hii, mbali na kuukaribia ubingwa, lakini kupata ushindi kutatuongezea nguvu ya kufanya vyema kwenye mechi zilizobakia za ligi na Kombe la FA," alisema Niyonzima.

Endapo Simba ambao ndio wenyeji wa mechi hiyo itashinda basi itakuwa inausogelea zaidi ubingwa kwa kufikisha pointi 64 na kuiacha Yanga ikiwa na pointi 57 zake. Hii ina maana kuwa vinara hao wa ligi wakishinda wataiacha Yanga kwa pointi saba, huku pia ikiwa imebakisha mechi mbili za viporo.

Kama Yanga itaondoka na ushindi katika mechi ya leo itakuwa imefikisha pointi 60, ikiiacha Simba ikibaki na pointi zake 61 na hivyo itakuwa imebakisha pointi moja tu kuifikia, ingawa bado Simba itakuwa na viporo viwili.

Kama zikitoka sare bado ni faida kwa Simba kwa sababu itakuwa na pointi 62, Yanga ikiwa na pointi 58, hivyo pengo la pointi nne litakuwa itabaki pale pale, pamoja na idadi ya mechi za viporo pia vitabaki viwili kama mwanzo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >